# القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

Juzuu - THREE (Tilka-Rusulu)

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy

250. Na walipotoka kupambana na Jaluti (mfalme wa hao maadui) na majeshi yake, walisema hao watu wa Taluti: "Mola wetu! Tumiminie subira, na uithibitishe miguu yetu, na utusaidie juu ya watu hawa makafiri."

وَلَمَّا بَرَزُوا لِجَالُوتَ وَجُنُودِهِ قَالُوا رَبَّنَا أَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا وَثَبِّتْ أَقْدَامَنَا وَانْصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٢٥٠﴾

251. Basi (hao watu wa Taluti) wakawaendesha mbio (hao maadui zao) kwa idhini ya Mwenyezi Mungu: na Daudi akamwua Jaluti, na Mwenyezi Mungu akampa (huyu Daudi) ufalme na hikima (Utume) na akamfundisha aliyoyapenda. Na kama Mwenyezi Mungu asingalizuia watu, baadhi yao kwa wengine, kwa yakini ardhi ingaliharibika. Lakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila (kubwa) juu ya walimwengu wote.

فَهَزَمُوهُمْ بِإِذْنِ اللَّهِ وَقَتَلَ دَاوُودُ جَالُوتَ وَآتَاهُ اللَّهُ الْمُلْكَ وَالْحِكْمَةَ وَعَلَّمَهُ مِمَّا يَشَاءُ ۗ وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ لَفَسَدَتِ الْأَرْضُ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ ذُو فَضْلٍ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٢٥١﴾

252. Hizi ni Aya za Mwenyezi Mungu, tunakusomea kwa haki. Na bila shaka wewe ni miongoni mwa (hao) Mitume (aliowaleta Mwenyezi Mungu).

تِلْكَ آيَاتُ اللَّهِ نَتْلُوهَا عَلَيْكَ بِالْحَقِّ ۚ وَإِنَّكَ لَمِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٢٥٢﴾

253. Mitume hao tumewafadhilisha baadhi yao zaidi kuliko wengine. Miongoni mwao wako ambao Mwenyezi Mungu alisema nao; na wengine akawapandisha katika vyeo vikubwa kabisa. Na Isa Mwana wa Mariyamu tukampa hoja zilizo wazi, na tukamtia nguvu kwa Roho Takatifu. Na kama Mwenyezi Mungu angalitaka wasingalipigana wale waliokuwa baada yao (baada ya hao Mitume) baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi. Lakini walihitalifiana. Kwa hivyo wako miongoni mwao walioamini, na wengine miongoni mwao waliokufuru. Na kama Mwenyezi Mungu angalipenda wasingalipigana; lakini Mwenyezi Mungu hufanya anayoyataka.

تِلْكَ الرُّسُلُ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ ۘ مِنْهُمْ مَنْ كَلَّمَ اللَّهُ ۖ وَرَفَعَ بَعْضَهُمْ دَرَجَاتٍ ۚ وَآتَيْنَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ الْبَيِّنَاتِ وَأَيَّدْنَاهُ بِرُوحِ الْقُدُسِ ۗ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا اقْتَتَلَ الَّذِينَ مِنْ بَعْدِهِمْ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمُ الْبَيِّنَاتُ وَلَٰكِنِ اخْتَلَفُوا فَمِنْهُمْ مَنْ آمَنَ وَمِنْهُمْ مَنْ كَفَرَ ۚ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا اقْتَتَلُوا وَلَٰكِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ ﴿٢٥٣﴾

---

245. Hapa watu wanahimizwa kutoa katika njia za kheri. Na kuwa hata ukitoa kidogo Mungu atakupa kikubwa huko Akhera na akutilie baraka hapa.

247. Hapa Mwenyezi Mungu anatia nguvu habari ya Ilimu na Siha. Mwenye Ilimu na Siha ndiye anayestahiki kupewa ukubwa wa kuendesha watu na mambo yao. Na ilimu haikamiliki katika kiwiliwili chenye siha mbovu. Uislamu unahimiza sana—katika Quran na Hadithi—juu ya kutafuta ilimu na kurai (kuchunga) siha.

Wamepotoa mahala pawili katika hii Aya waliyosema kuwa ni Aya ya 248. Kwanza kusema kwao kuwa:

(a) Talut "mfalme mmoja wa Kiisraeli, aliyekuwako miaka mia mbili kabla ya Nabii Daud". Mwenyezi Mungu kasema hapa kuwa katika vita hivi alivyopiganisha Mfalme Talut alipigana kwa ushujaa mkubwa, mtu aliyekuwa akiitwa Daud, akamwua Jalut (mfalme wa maadui) na akapewa yeye ufalme, kisha akapata na Utume. Wao wanajifanya wanajua kuliko Mwenyewe Mwenyezi Mungu. Wanasema kuwa Talut alikuwa miaka mia mbili kabla ya kuzaliwa Nabii Daud.

(b) Tabuti (na wameliharibu vile vile katika 249) Wakasema kuwa Tabuti maana yake Moyo. Wamepindua hivi, na hali ya kuwa wanajua kuwa Tabuti maana yake Sanduku, kama walivyofasiri wafasiri wa Qurani w te, na wafasiri wa maneno magumu ya Qurani wote, na wenye kufasiri maneno ya Kiarabu yo yote. Wote wamesema kuwa Tabuti maana yake Sanduku. Na Mwenyezi Mungu ndivyo alivyosema hapa kuwa "Atakuleteeni lile Sanduku (lenu) ambalo mna ndani yake kituliza nyoyo zenu, kitokacho kwa Mola wenu, na mna masazo ya yale waliyoyaacha watu wa Musa na watu wa Harun." Hilo ni Sanduku ambalo ndani yake zilikuwamo hizo mbao ambazo ndani yake zimeandikwa zile amri kumi alizoteremshiwa Nabii Musa, na yalikuwamo ndani yake masazo

254. Enyi mlioamini! Toeni katika vile tulivyokupeni kabla haijafika Siku ambayo hapatakuwa kujikomboa wala urafiki (wa kusaidiana) wala uombezi. Na waliokufuru ndio waliojidhulumu (kweli kweli).

255. Mwenyezi Mungu hakuna mola ila Yeye, (na) ndiye Mwenye uhai wa maisha, Msimamia kila jambo. Kusinzia hakumshiki wala kulala. Ni Vyake (peke yake vyote) vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi. Na nani huyo awezaye kuombea mbele Yake (Mungu) bila ya idhini yake? Anayajua yaliyo mbele yao (viumbe) na (yaliyo) nyuma yao; wala (hao viumbe) hawalijui lo lote katika (yaliyo katika) ilimu Yake (Mwenyezi Mungu) ila kwa alipendalo (Mwenyewe). Enzi yake imeenea mbingu; na ardhi; wala kuvilinda hivyo hakumshindi; na Yeye (peke yake) ndiye aliye juu na ndiye aliye Mkuu.

256. Hakuna kulazimishwa (mtu kuingia) katika dini. Uongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anayemkataa shetani na akamwamini Mwenyezi

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ أَنفِقُوا۟ مِمَّا رَزَقْنَٰكُم مِّن
قَبْلِ أَن يَأْتِىَ يَوْمٌ لَّا بَيْعٌ فِيهِ وَلَا خُلَّةٌ وَلَا شَفَٰعَةٌ ۗ
وَٱلْكَٰفِرُونَ هُمُ ٱلظَّٰلِمُونَ ۝
ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلْحَىُّ ٱلْقَيُّومُ ۚ لَا تَأْخُذُهُۥ
سِنَةٌ وَلَا نَوْمٌ ۚ لَّهُۥ مَا فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِى
ٱلْأَرْضِ ۗ مَن ذَا ٱلَّذِى يَشْفَعُ عِندَهُۥٓ إِلَّا
بِإِذْنِهِۦ ۚ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ ۖ
وَلَا يُحِيطُونَ بِشَىْءٍ مِّنْ عِلْمِهِۦٓ إِلَّا بِمَا شَآءَ ۚ
وَسِعَ كُرْسِيُّهُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ ۖ وَلَا يَـُٔودُهُۥ
حِفْظُهُمَا ۚ وَهُوَ ٱلْعَلِىُّ ٱلْعَظِيمُ ۝
لَآ إِكْرَاهَ فِى ٱلدِّينِ ۖ قَد تَّبَيَّنَ ٱلرُّشْدُ مِنَ ٱلْغَىِّ ۚ

---

mengine ya vitu vitukufu vya dini alivyoviwacha Nabii Musa na Nabii Harun. Walikuwa Mayahudi kila wakenda vitani huenda (hwenda) na sanduku lao hili, wanatabaruku nalo. Wakiwa nalo sanduku hilo hutua nyoyo zao, wakaona watashinda tu. Mwisho wakashindwa na watu wa Falastin (Palestine) na wakawanyanganya sanduku lao hilo. Wakavunjika nyoyo kweli kweli. Sasa ndio wanapewa bishara kuwa wakimkubali mfalme huyo – Talut – litawarejelea sanduku lao na kila kilichokuwamo humo. Wao Makadiyani wanasema maana ya Tabuti ni moyo. Kwa tafsiri yao hiyo ingekuwa maana ya Aya hii: "Atakuleteeni moyo, ambao ndani yake mna utulivu (kituliza nyoyo zenu) unaotokana kwa Mola wenu, na masazo ya yale waliyoyaacha watu wa Musa na Harun." Basi maneno haya husema mwenye akili yake! Au husema mbabaishaji kama wao? Hapana shaka kuwa hasemi maneno haya ila m-babaishaji. ·Watababaika wenyewe Inshaallah maisha.

Wakasingizia kuwa maneno haya kayafuata imam Ar Raghibul Isfahany na ndivyo alivyofasiri; kama ilivyo katika *Mufradat* (ya Raghibul Isfahany), na yamo katika Kamus la Lane (Arabic-English Lexicon by E.W. Lane). Wanataja vitabu namna hivi kwa kuona kuwa hawataweza watu wa pande hizi kuvipata vitabu hivi kwani haviuzwi kabisa katika maduka ya Vitabu ya Mashariki ya Afrika na Magharibi yake. Wamehizika basi ile ile hizaya ya bibo — kichwa chini, miguu juu. Ukweli ni huu: Ameitaja tu kauli hii Arraghib akasema: "Kuna wengine wamesema kuwa ni moyo." Hakusema yeye kuwa hiyo ndiyo tafsiri yake barabara, kama walivyofahamisha wao Makadiyani kuwa hiyo ndiyo aliyoitilia nguvu Ar Raghibul Isfahany katika kitabu chake *(Al Mufradat)*. Uwongo wao na upotezaji wao hawa ni mwingi kweli kweli.

249. Kutii (Taa) ni kitu kikubwa kabisa katika kutengenea mambo ya watu. Watu wasiokuwa na Taa ya kutii mambo yao, huharibikiwa tu. Na hapa anatoka Mfalme huyu. Talut na jeshi kubwa, wala halijui utiifu wake, basi Mwenyezi Mungu ndiyo akamwambia awafanyie mtihani huu wa kutokunywa mpaka kukata kiu. Wasiotii asiwachukue kwenda huko kwenye midani ya vita wasije wakakhalifu watakayoambiwa.

250. Tazama hamu yao ya kutaka kuyapinga yaliyomo katika Qurani. Wanasema katika Aya hii waliyoifanya kuwa ya 251. Wamesema: "Jaluti mradi wake si mtu mmoja, bali taifa la watu." Basi vipi Mungu angesema "Jaluti na majeshi yake?" Basi; hamu yao wao ni kutaka kuikoroga Qurani tu kwa kila njia.

251. Nabii Daudi alikuwa ni askari katika hilo jeshi la mfalme Taluti. Akapigana kwa nia nzuri na ushujaa mkubwa kabisa hata akamwua mfalme wa hao maadui (makafiri) aliyekuwa akiitwa Jaluti. Basi Mwenyezi Mungu akampa Utume na Ufalme na mengineyo kwa hayo aliyofanya. Jitahidi ndiyo Mungu akupe. Sio ukinge mikono tu upewe.

Na hapa anaonyesha Mwenyezi Mungu kuwa watu wakitaadi (wakifanya jeuri kubwa) Mwenyezi Mungu huleta watu wengine wakawapiga wakawatawala hao. Tumeona, na tutazidi kuona. Na tunaomba salama.

253. Aya hii inaonyesha kuwa Mitume daraja zao ni mbali mbali kwa Mwenyezi Mungu kama Binaadamu wengine na Malaika na Majini na vinginevyo. Wanazidiana kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na kwa amali zao

Mungu, bila shaka yeye ameshika kishiko chenye nguvu kisichokuwa na kuvunjika. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye kusikia mwenye kujua.

257. Mwenyezi Mungu ni mlinzi wa wale walioamini. Huwatoa katika giza na kuwaingiza katika mwangaza. Lakini waliokufuru, walinzi wao ni mashetani. Huwatoa katika mwangaza na kuwaingiza katika giza. Hao ndio watu wa Motoni, humo watakaa milele.

258. Hukumsikia yule aliyehojiana na Ibrahimu juu ya Mola wake kwa sababu Mwenyezi Mungu alimpa ufalme? Ibrahimu aliposema: "Mola wangu ni yule ambaye huhuisha na hufisha," yeye akasema: "Mimi pia nahuisha na kufisha." Ibrahimu akasema: "Mwenyezi Mungu hulichomozesha jua mashariki, basi wewe lichomozeshe magharibi." Akafedheheka yule aliyekufuru; na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu.

259. Au kama yule aliyepita karibu na mji uliokuwa umekufa akasema: "Mwenyezi Mungu atauhuisha vipi (mji) huu (na watu wake) baada ya kufa kwake?" Basi Mwenyezi Mungu alimfisha kwa miaka mia, kisha akamfufua akamwuliza: "Umekaa muda gani?" Akasema: "Nimekaa muda wa siku moja au sehemu ya siku." (Mwenyezi Mungu) akasema: "Bali umekaa miaka mia; nawe tazama chakula chako na vinywaji vyako, havikuharibika.

فَمَنْ يَّكْفُرْ بِالطَّاغُوْتِ وَيُؤْمِنْ بِاللّٰهِ فَقَدِ
اسْتَمْسَكَ بِالْعُرْوَةِ الْوُثْقٰى لَا انْفِصَامَ لَهَا ؕ
وَاللّٰهُ سَمِيْعٌ عَلِيْمٌ ﴿٢٥٦﴾
اَللّٰهُ وَلِيُّ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا يُخْرِجُهُمْ مِّنَ الظُّلُمٰتِ
اِلَى النُّوْرِ ؕ وَالَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اَوْلِيٰٓـُٔهُمُ الطَّاغُوْتُ
يُخْرِجُوْنَهُمْ مِّنَ النُّوْرِ اِلَى الظُّلُمٰتِ ؕ
اُولٰٓئِكَ اَصْحٰبُ النَّارِ ۚ هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ﴿٢٥٧﴾
اَلَمْ تَرَ اِلَى الَّذِيْ حَآجَّ اِبْرٰهٖمَ فِيْ رَبِّهٖٓ اَنْ
اٰتٰىهُ اللّٰهُ الْمُلْكَ ۘ اِذْ قَالَ اِبْرٰهٖمُ رَبِّيَ الَّذِيْ
يُحْيٖ وَيُمِيْتُ ۙ قَالَ اَنَا اُحْيٖ وَاُمِيْتُ ؕ قَالَ
اِبْرٰهٖمُ فَاِنَّ اللّٰهَ يَاْتِيْ بِالشَّمْسِ مِنَ الْمَشْرِقِ فَاْتِ
بِهَا مِنَ الْمَغْرِبِ فَبُهِتَ الَّذِيْ كَفَرَ ؕ
وَاللّٰهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظّٰلِمِيْنَ ﴿٢٥٨﴾
اَوْ كَالَّذِيْ مَرَّ عَلٰى قَرْيَةٍ وَّهِيَ خَاوِيَةٌ عَلٰى
عُرُوْشِهَا ۚ قَالَ اَنّٰى يُحْيٖ هٰذِهِ اللّٰهُ بَعْدَ مَوْتِهَا ۚ
فَاَمَاتَهُ اللّٰهُ مِائَةَ عَامٍ ثُمَّ بَعَثَهٗ ؕ قَالَ كَمْ لَبِثْتَ ؕ
قَالَ لَبِثْتُ يَوْمًا اَوْ بَعْضَ يَوْمٍ ؕ قَالَ بَلْ لَّبِثْتَ

walizofanya ambazo si sawa sawa. Za wengine ni kubwa zaidi au nyingi zaidi kuliko za wenziwao.

Na hapa Mwenyezi Mungu amewataja watatu katika hao Mitume wakubwa kabisa. Naye ni huyo Aliyesemezwa na Mwenyezi Mungu. Naye ni Nabii Musa; aliyepewa hoja zilizo wazi . . . Naye ni Nabii Isa. Na Aliyepandishwa vyeo vikubwa kabisa. Naye ni Nabii Muhammad. Na vile vile katika hao wakubwa kabisa ni Nabii Ibrahimu na Nabii Nuhu kama ilivyofahamishwa katika Aya nyenginezo kama Aya ya 7 ya *Suratil Ahzab* inavyosema. Na anayewekwa mbele katika hao ni (a) Nabii Muhammad (b) Kisha Nabii Ibrahimu (c) Tena Nabii Musa (d) Baadaye Nabii Isa (e) Na hatimaye Nabii Nuhu.

Na huyo Roho Mtakatifu ni Jibril anayewaletea Wahyi Mitume. Basi kwa Mitume wengine kateremka mara nyingi zaidi kuliko kwa Mitume wengine.

Na aliposema Mwenyezi Mungu 'Na kama Mungu angalitaka ...' ni kuonyesha kuwa Mwenyezi Mungu hakuwaumba Wanaadamu umbo la Malaika. Na angetaka angewaumba hivyo (Kimalaika); wakawa wanakwenda mwendo ule ule waliowekewa, hawakhalifu hata kidogo, ikawa wanafanya mema tu. Lakini Binaadamu kawaumba akawapa huria ya kufanya jema na baya. Na angalitaka kuwaumba Kimalaika asingeshindwa. Lakini Mwenyewe Mwenyezi Mungu katafautisha baina ya viumbe vyake — Malaika kawaumba wana akili na Hawana matamanio. Akawaumba wanyama kuwa wana matamanio lakini Hawana akili (wana utambuzi mdogo tu). Na akawaumba Binaadamu na yote mawili. Wana matamanio na wana akili ya kupima baina ya jema na baya na baina ya jema na jema zaidi na baina ya baya na baya zaidi — wafanye wanalolitaka bila kufungika kwa moja wapo. Na hayo Matamanio yao ndiyo yanayowapelekea kutowafikiana. Na angetaka Mwenyezi Mungu asingewaumba hivi. Basi Mwanaadamu akipigana na Matamanio yake akafika katika utakatifu unaokurubia wa Kimalaika huwa bora kuliko hao Malaika. Na akitawaliwa na Matamanio yake anakuwa kama mnyama, na zaidi kuliko mnyama kwani yeye ana hatamu ya akili, naye hataki kuzuilia kasi zake kwa hatamu hizo.

254. Wafasiri wote wanasema kuwa muradi wa tamko la *Man Kallamallahu* (aliyesemezwa na Mwenyezi

Na mtazame punda wako (amekuwa mifupa mitupu iliyolikalika). Na ili tukufanye uwe hoja kwa watu (ndio tumekufufua hivi). Na itazame mifupa (ya punda wako) jinsi tunavyoinyanyua, kisha tunaivisha nyama." Basi yalipombainikia (haya yule aliyefufuliwa) alinena: 'Najua kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu."

مِائَةَ عَامٍ فَانْظُرْ إِلَىٰ طَعَامِكَ وَشَرَابِكَ لَمْ يَتَسَنَّهْ ۖ وَانْظُرْ إِلَىٰ حِمَارِكَ وَلِنَجْعَلَكَ آيَةً لِلنَّاسِ ۖ وَانْظُرْ إِلَى الْعِظَامِ كَيْفَ نُنْشِزُهَا ثُمَّ نَكْسُوهَا لَحْمًا ۚ فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهُ قَالَ أَعْلَمُ أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٥٩﴾

260. Na (kumbuka) Ibrahimu aliposema: "Mola wangu! Nionyeshe jinsi utakavyofufua wafu." (Mwenyezi Mungu) akasema: "Huamini?" Akasema: "La, (naamini), lakini (nataka kuona hayo) ili moyo wangu utulie (zaidi)." Akasema: "Basi chukua ndege wane na uwazoeshe kwako (uwadhibiti vizuri sura zao hata wasikupotee po pote unapowaona), kisha (wachinje) uweke juu ya kila jabali sehemu katika wao. Kisha waite, watakujia mbio. Na ujue ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, na Mwenye hikima."

وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ أَرِنِي كَيْفَ تُحْيِي الْمَوْتَىٰ ۖ قَالَ أَوَلَمْ تُؤْمِنْ ۖ قَالَ بَلَىٰ وَلَٰكِنْ لِيَطْمَئِنَّ قَلْبِي ۖ قَالَ فَخُذْ أَرْبَعَةً مِنَ الطَّيْرِ فَصُرْهُنَّ إِلَيْكَ ثُمَّ اجْعَلْ عَلَىٰ كُلِّ جَبَلٍ مِنْهُنَّ جُزْءًا ثُمَّ ادْعُهُنَّ يَأْتِينَكَ سَعْيًا ۚ وَاعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٢٦٠﴾

261. Mfano wa wale wanaotoa mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyotoa mashuke saba; ikawa katika kila shuke pana punje mia. Na Mwenyezi Mungu humzidishia

مَثَلُ الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ كَمَثَلِ حَبَّةٍ أَنْبَتَتْ سَبْعَ سَنَابِلَ فِي كُلِّ سُنْبُلَةٍ

---

Mungu) ni Nabii Musa. Na muradi wa tamko la *Waayyadnaahu Biruhil Qudus* (Tukamtia nguvu kwa Roho Takatifu) ni Nabii Isa. Na muradi wa *Warafaa Baadhahum Darajaat* (Akawainua wengine daraja kubwa kabisa) ni Nabii Muhammad. Wao wamepachikiapachikia ili wafanye ile kazi yao ya kuwapoteza Waislamu. Lakini hawakuweza kujidhihirisha sana. Walipachika hayo katika ile paragraph ya mwisho iliyoanzia hivi: "Miongoni mwao wako ambao Mwenyezi Mungu alisema nao."

255. Aya hii huitwa *Ayatul Kursy*. Aya tukufu kabisa. Anahimizwa kila Mwislamu Kuyaweka maana ya Aya hii mbele ya macho yake daima—ili asimwone *Muqaddim* wala *Muakhkhir* ila Mwenyewe tu Mwenyezi Mungu Subhanahuu Wataala. Na mahala pengi katika Hadithi za Mtume amehimizwa mtu kuisoma, kama (a) baada ya kutoa salamu katika Sala (b) Kabla ya kulala (c) Anapotoka nje (d) Anapoingia ndani (e) Anapokuwa na khofu ya kuogopa vinavyoonekana na visivyoonekana.

256. Baadhi ya Waarabu wa Madina kabla hakwenda Nabii Muhammad huko walikuwa wanafuata dini ya Kiyahudi. Lakini wengi wao wakiabudu masanamu. Ulipokuja Uislamu, takriba wote hao waliokuwa wakiabudu masanamu walisilimu. Ama katika wale waliokuwa na dini ya Kiyahudi walisilimu kidogo tu, na wengine wakasalia na Mayahudi japo kuwa ni Waarabu. Basi baba zao waliosilimu na ndugu zao na wakubwa wao na waume zao na bwana zao walitaka wawatie katika Uislamu kwa nguvu. Basi wakakatazwa hapa na Mwenyezi Mungu kuwa: Hakuna ruhusa kumkalifisha asiyetaka, kila mtu kapewa akili ya kutambua jema na baya. Basi akifuata upotofu hiari yake mwenyewe, na Mungu atamtesa Akhera huko, si hapa.

Basi umefedheheka hapa uwongo wa wale wanaozua kuwa Uislamu unalazimisha watu kwa nguvu kuingia katika dini hiyo japo wenyewe hawataki. Basi Uislamu gani huo wanaousingizia hivyo? Na Uislamu ni huu uliyomo katika Quran—mweupe, hauna kificho cho chote. Lakini anayetaka kukutukana hakuchagulii tusi.

258. Katika zama za Nabii Ibrahimu alikuwako mfalme jabari ambaye alidai Uungu, na raia zake wakamwabudu. Alipokuja Nabii Ibrahimu kufundisha dini ya haki na kuwa huyo si Mungu, alimwambia Nabii Ibrahimu 'Kwani huyo Mungu wa haki hufanya nini?' Akamwambia 'Huhuisha na kufisha.' Akajitia pambani—kufanya kama kwamba hakufahamu muradi wa Nabii Ibrahimu—akamwambia 'Na mimi pia nafanya kazi hii. Nitazame ninavyoifanya.' Pale pale akaamrisha waletwe watu wawili waliostahiki kuuawa, akaamrisha auawe mmoja katika hao na mmoja asamehewe. Yakafanywa hayo. Akamwambia Nabii Ibrahimu 'Umeonaje? Si nimehuisha na nimefisha?'

Nabii Ibrahimu alipomwona anajitia pambani kusudi alimpa jambo ambalo hawezi kulitilia pambani;

amtakaye, (zaidi kuliko hivi), na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa mkubwa (na) Mwenye kujua.

262. Wale wanaotoa mali zao kwa njia ya Mwenyezi Mungu, kisha hawafuatishii — waliyoyatoa — masumbulizi wala udhia, wao wana ujira wao kwa Mola wao, wala haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.

263. Kauli njema na kumsamehe (anayekukosa) ni bora kuliko sadaka inayofuatishwa na udhia. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mkwasi na mpole kwa (viumbe vyake).

264. Enyi mlioamini! Msiharibu sadaka zenu kwa masumbulizi na udhia; kama yule anayetoa mali yake kwa kuwaonyesha watu, wala hamwamini Mwenyezi Mungu wala siku ya mwisho. Basi hali yake ni kama hali ya jabali ambalo juu yake pana udongo, kisha ikalifikia (jabali hili) mvua kubwa (ikasukuma udongo wote huo) na ikaliacha tupu. Basi hawatakuwa na uweza (wa kupata) cho chote katika walivyovichuma; na Mwenyezi Mungu hawaongozi watu makafiri.

265. Na mfano wa wale wanaotoa mali zao kwa kuitafuta radhi ya Mwenyezi Mungu na kujithibitisha nafsi zao (katika dini yake), ni kama mfano wa bustani iliyo mahali pa juu, ikaifikia mvua kubwa na ikaleta mazao yake mara mbili na zaidi, (kuliko ada yake); na kama haifikiwi na mvua kubwa basi mvua ndogo (huitoshea). Na Mwenyezi Mungu anayaona mnayoyatenda.

266. Je! Mmoja wenu anapenda kuwa na bustani ya mitende na mizabibu ipitayo mito mbele yake, naye humo hupata mazao ya kila namna, na uzee ukamfikia, kisha ana watoto walio dhaifu; mara kimbunga chenye moto kikaifikia, ikaungua? (Anapenda mtu haya?) Hivi ndivyo Mwenyezi Mungu anavyokubainishieni Aya (zake) ili mpate kufikiri.

267. Enyi mlioamini! Toeni katika vile vizuri mlivyovichuma, na katika vile tulivyokutoleeni katika ardhi. Wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya, hali nyinyi wenyewe msingevipokea isipokuwa kwa kutoviangalia (Basi Mungu atapokea kibaya?). Basi jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Mkwasi na asifiwaye.

مِّائَةُ حَبَّةٍ ۗ وَاللَّهُ يُضَاعِفُ لِمَن يَشَاءُ ۗ
وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٦١﴾
الَّذِينَ يُنفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ثُمَّ لَا يُتْبِعُونَ
مَا أَنفَقُوا مَنًّا وَلَا أَذًى ۙ لَّهُمْ أَجْرُهُمْ عِندَ
رَبِّهِمْ ۚ وَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٢٦٢﴾
قَوْلٌ مَّعْرُوفٌ وَمَغْفِرَةٌ خَيْرٌ مِّن صَدَقَةٍ يَتْبَعُهَا
أَذًى ۗ وَاللَّهُ غَنِيٌّ حَلِيمٌ ﴿٢٦٣﴾
يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تُبْطِلُوا صَدَقَاتِكُم
بِالْمَنِّ وَالْأَذَىٰ كَالَّذِي يُنفِقُ مَالَهُ رِئَاءَ
النَّاسِ وَلَا يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۖ فَمَثَلُهُ
كَمَثَلِ صَفْوَانٍ عَلَيْهِ تُرَابٌ فَأَصَابَهُ وَابِلٌ
فَتَرَكَهُ صَلْدًا ۖ لَّا يَقْدِرُونَ عَلَىٰ شَيْءٍ مِّمَّا
كَسَبُوا ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ ﴿٢٦٤﴾
وَمَثَلُ الَّذِينَ يُنفِقُونَ أَمْوَالَهُمُ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ
اللَّهِ وَتَثْبِيتًا مِّنْ أَنفُسِهِمْ كَمَثَلِ جَنَّةٍ بِرَبْوَةٍ
أَصَابَهَا وَابِلٌ فَآتَتْ أُكُلَهَا ضِعْفَيْنِ فَإِن لَّمْ
يُصِبْهَا وَابِلٌ فَطَلٌّ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٢٦٥﴾
أَيَوَدُّ أَحَدُكُمْ أَن تَكُونَ لَهُ جَنَّةٌ مِّن نَّخِيلٍ وَ
أَعْنَابٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ لَهُ فِيهَا
مِن كُلِّ الثَّمَرَاتِ وَأَصَابَهُ الْكِبَرُ وَلَهُ ذُرِّيَّةٌ
ضُعَفَاءُ فَأَصَابَهَا إِعْصَارٌ فِيهِ نَارٌ فَاحْتَرَقَتْ ۗ
كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمُ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَتَفَكَّرُونَ ﴿٢٦٦﴾ ع
يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَنفِقُوا مِن طَيِّبَاتِ مَا كَسَبْتُمْ
وَمِمَّا أَخْرَجْنَا لَكُم مِّنَ الْأَرْضِ ۖ وَلَا تَيَمَّمُوا
الْخَبِيثَ مِنْهُ تُنفِقُونَ وَلَسْتُم بِآخِذِيهِ إِلَّا أَن
تُغْمِضُوا فِيهِ ۚ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿٢٦٧﴾

---

akamwambia habari hii ya kutolesha Mwenyezi Mungu jua Mashariki .... Yeye alitoleshe Magharibi kama yeye ni Mungu pia. Hapo akadahadari asijue la kutenda wala la kunena.

268. Shetani anakuogopesheni ufukara na anakuamrisheni ubakhili; na Mwenyezi Mungu anakuahidini msamaha utokao kwake na ihsani (kubwa pindi mkitoa); na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa mkubwa na Mwenye kujua

الشَّيْطٰنُ يَعِدُكُمُ الْفَقْرَ وَيَأْمُرُكُمْ بِالْفَحْشَآءِ ۚ
وَاللّٰهُ يَعِدُكُمْ مَّغْفِرَةً مِّنْهُ وَفَضْلًا ۗ وَاللّٰهُ
وَاسِعٌ عَلِيْمٌ ﴿٢٦٨﴾

269. (Mungu) humpa hikima (akili yenye nafuu) amtakaye, na aliyepewa hikima bila shaka amepewa kheri nyingi. Na hawakumbuki ila wenye akili.

يُّؤْتِي الْحِكْمَةَ مَنْ يَّشَآءُ ۚ وَمَنْ يُّؤْتَ الْحِكْمَةَ
فَقَدْ أُوْتِيَ خَيْرًا كَثِيْرًا ۗ وَمَا يَذَّكَّرُ
إِلَّآ أُولُوا الْأَلْبَابِ ﴿٢٦٩﴾

270. Na cho chote mtoacho au nadhiri mnazoweka basi Mwenyezi Mungu anajua. Na madhalimu (wanaodhulumu nafsi zao kwa kutotoa) hawatakuwa na wasaidizi.

وَمَآ أَنْفَقْتُمْ مِّنْ نَّفَقَةٍ أَوْ نَذَرْتُمْ مِّنْ نَّذْرٍ
فَإِنَّ اللّٰهَ يَعْلَمُهُ ۗ وَمَا لِلظّٰلِمِيْنَ مِنْ أَنْصَارٍ ﴿٢٧٠﴾

271. Kama mkitoa sadaka kwa dhahiri ni vizuri; na kama mkitoa kwa siri na kuwapa mafakiri, basi huo ni ubora zaidi kwenu; na atakuondoleeni (sehemu ya) maovu yenu (mkifanya hivyo); na Mwenyezi Mungu anazo habari za (yote) mnayoyatenda.

إِنْ تُبْدُوا الصَّدَقٰتِ فَنِعِمَّا هِيَ ۚ وَإِنْ تُخْفُوْهَا
وَتُؤْتُوْهَا الْفُقَرَآءَ فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ۚ وَيُكَفِّرُ عَنْكُمْ
مِّنْ سَيِّاٰتِكُمْ ۗ وَاللّٰهُ بِمَا تَعْمَلُوْنَ خَبِيْرٌ ﴿٢٧١﴾

272. Si juu yako kuwaongoa; lakini Mwenyezi Mungu humwongoa amtakaye. (Juu yako ni kuongoza tu). Na mali yo yote mtakayoyatoa ni (faida) kwa nafsi zenu. Wala msitoe ila kwa kutafuta radhi ya Mwenyezi Mungu. Na mali yo yote mtakayotoa mtarudishiwa kamili (thawabu zake), wala hamtadhulumiwa.

لَيْسَ عَلَيْكَ هُدٰىهُمْ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ يَهْدِيْ مَنْ
يَّشَآءُ ۗ وَمَا تُنْفِقُوْا مِنْ خَيْرٍ فَلِأَنْفُسِكُمْ ۗ وَمَا
تُنْفِقُوْنَ إِلَّا ابْتِغَآءَ وَجْهِ اللّٰهِ ۗ وَمَا تُنْفِقُوْا
مِنْ خَيْرٍ يُّوَفَّ إِلَيْكُمْ وَأَنْتُمْ لَا تُظْلَمُوْنَ ﴿٢٧٢﴾

273. (Wapewe hizo sadaka) mafakiri waliozuiwa katika njia za Mwenyezi Mungu, wasioweza kwenda huko na huko katika ardhi (kufanya kazi ya kutafuta riziki); asiyewajua hali zao anawadhania kuwa ni matajiri kwa sababu ya kujizuia kwao (na kuomba). Utawafahamu (kuwa wahitaji) kwa alama zao (zinazoonyesha ufakiri, lakini) hawawaombi watu wakafanya ung'ang'anizi. Na mali yo yote mnayoyatoa, basi kwa yakini Mwenyezi Mungu anayajua (atakulipeni).

لِلْفُقَرَآءِ الَّذِيْنَ أُحْصِرُوْا فِيْ سَبِيْلِ اللّٰهِ لَا
يَسْتَطِيْعُوْنَ ضَرْبًا فِي الْأَرْضِ يَحْسَبُهُمُ الْجَاهِلُ
أَغْنِيَآءَ مِنَ التَّعَفُّفِ ۚ تَعْرِفُهُمْ بِسِيْمٰهُمْ ۚ لَا يَسْـَٔلُوْنَ
النَّاسَ إِلْحَافًا ۗ وَمَا تُنْفِقُوْا مِنْ خَيْرٍ فَإِنَّ اللّٰهَ بِهٖ
عَلِيْمٌ ﴿٢٧٣﴾

274. Wale watowao mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhahiri, wana ujira wao kwa Mola wao; wala haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.

اَلَّذِيْنَ يُنْفِقُوْنَ أَمْوَالَهُمْ بِالَّيْلِ وَالنَّهَارِ سِرًّا وَّ
عَلَانِيَةً فَلَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۚ وَلَا خَوْفٌ
عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُوْنَ ﴿٢٧٤﴾

---

259. Mtu huyo na wenziwe wa zama zake walikuwa wakikataa katakata kuwa viumbe watafufuliwa. Wakiona kuwa jambo hilo ni muhali kabisa. Basi Mwenyezi Mungu alimwonyesha hayo katika nafsi yake ili ende akawahadithie hao wenziwe waliokuwa pamoja na yeye, na yeye akawa mkubwa wao. Na aliyewafikilishia ujumbe wa Mungu huu ni Mtume aliyekuwa zama zao.

260. Nabii Ibrahimu alitamani aone namna gani watafufuka waliokufa—ili izidi nguvu imani yake. Basi Mwenyezi Mungu alimwamrisha awachinje ndege wane wa kabila mbali mbali. Kisha aviparaganyeparaganye viungo vyao—vya huyu vyende kwa yule na vya yule vyende kwa huyo. Kisha avigawe viungo hivyo sehemu 4. Kila sehemu aiweke katika jabali moja. Kisha awete. Ataona kila kiungo cha ndege mahsusi kinakimbilia viungo

275. Wale wanaokula riba, hawasimami (kuendesha yao) ila kama anavyosimama yule ambaye Shetani kamzuga kwa kumsawaa; (wako mbioni tu, hawana kituo). (Na) haya ni kwa sababu wamesema, "Biashara ni kama riba", hali Mwenyezi Mungu ameihalalisha biashara na kaiharimisha riba. Na aliyefikiwa na mauidha kutoka kwa Mola wake (ya huku kukatazwa riba), kisha akajizuia, basi yamekwisha mthibitikia yale (mali) yaliyopita (aliyokwisha yapata); na hukumu yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Lakini wanaorejea (kula riba) basi hao ndio watu wa Motoni, humo watakaa milele.

ٱلَّذِينَ يَأْكُلُونَ ٱلرِّبَوٰا۟ لَا يَقُومُونَ إِلَّا كَمَا يَقُومُ
ٱلَّذِى يَتَخَبَّطُهُ ٱلشَّيْطَٰنُ مِنَ ٱلْمَسِّ ۚ ذَٰلِكَ
بِأَنَّهُمْ قَالُوٓا۟ إِنَّمَا ٱلْبَيْعُ مِثْلُ ٱلرِّبَوٰا۟ ۗ وَأَحَلَّ ٱللَّهُ
ٱلْبَيْعَ وَحَرَّمَ ٱلرِّبَوٰا۟ ۚ فَمَن جَآءَهُۥ مَوْعِظَةٌ مِّن رَّبِّهِۦ
فَٱنتَهَىٰ فَلَهُۥ مَا سَلَفَ وَأَمْرُهُۥٓ إِلَى ٱللَّهِ ۖ وَمَنْ عَادَ
فَأُو۟لَٰٓئِكَ أَصْحَٰبُ ٱلنَّارِ ۖ هُمْ فِيهَا خَٰلِدُونَ ﴿٢٧٥﴾

276. Mwenyezi Mungu huyafutia (baraka mali ya) riba: na huyatia baraka (mali yanayotolewa) sadaka. Na Mwenyezi Mungu hampendi kila kafiri (na) afanyae dhambi.

يَمْحَقُ ٱللَّهُ ٱلرِّبَوٰا۟ وَيُرْبِى ٱلصَّدَقَٰتِ ۗ وَٱللَّهُ لَا يُحِبُّ
كُلَّ كَفَّارٍ أَثِيمٍ ﴿٢٧٦﴾

277. Hakika wale walioamini na kufanya vitendo vizuri na kusimamisha Sala na kutoa Zaka, wao watapata ujira wao kwa Mola wao, wala haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika.

إِنَّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ وَأَقَامُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ
وَءَاتَوُا۟ ٱلزَّكَوٰةَ لَهُمْ أَجْرُهُمْ عِندَ رَبِّهِمْ وَلَا خَوْفٌ
عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٢٧٧﴾

278. Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na acheni yaliyobakia katika riba, ikiwa mmeamini.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ وَذَرُوا۟ مَا بَقِىَ مِنَ
ٱلرِّبَوٰٓا۟ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴿٢٧٨﴾

279. Na kama hamtafanya (hivyo), basi fahamuni mtakuwa na vita na Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na mkiwa mmetubu, basi mtapata rasilmali zenu; msidhulumu wala msidhulumiwe.

فَإِن لَّمْ تَفْعَلُوا۟ فَأْذَنُوا۟ بِحَرْبٍ مِّنَ ٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ ۖ
وَإِن تُبْتُمْ فَلَكُمْ رُءُوسُ أَمْوَٰلِكُمْ لَا تَظْلِمُونَ
وَلَا تُظْلَمُونَ ﴿٢٧٩﴾

280. Na kama (mkopi) ana dhiki, basi (mdai) angoje mpaka afarijike. Na kama nyinyi (mnaodai

وَإِن كَانَ ذُو عُسْرَةٍ فَنَظِرَةٌ إِلَىٰ مَيْسَرَةٍ ۚ

---

vyengine vya ndege huyo. Pale pale wakawa ndege wahai kama walivyokuwa. Na wengine wanafasiri vyengine.

Tazama khiana ya Makadiyani katika kuifasiri Aya hii waliyoifanya kuwa ni ya 261. Wamesema: *"Fasurhunna ilaika."* Maneno haya yametafsiriwa "Uwazoezeshe kwako" siyo "Uwakatekate na uwakoroge" kama walivyofasiri baadhi ya watu. Makadiyani wana yakini kuwa Aya hii imefasiriwa kwa tafsiri zote mbili hizo, bali hiyo tafsiri ya kukatakata na kukoroga ndiyo iliyofuatwa na wafasiri wengi zaidi—na zote mbili sawa sawa. Wao wanakataa wanasema kuwa hiyo tafsiri ya pili "Siyo." Na yote haya ni kule kukanusha kwao uweza wa Mwenyezi Mungu wa kufufua—hapa ulimwenguni—baadhi ya waliokufa; kwa ajili ya kuonyesha miujiza yake Mwenyewe Mwenyezi Mungu. Na tumeyavunja haya katika Aya ya 56 ya *Suratul Baqarah*. Wamesema "Siyo", na hali ya kuwa tafsiri hiyo imetajwa katika vitabu vyote vya (1) tafsiri ya Quran, kama *Jalaleyn*, na vitabu vyote vya (2) kufasiri maneno magumu ya Quran, kama *Al Mufradat* kama ilivyotaja ile tafsiri ya kwanza pia, na vitabu vyote vya (3) kufasiri maneno ya Kiarabu (Madictionary) vilivyotungwa na Waislamu, kama *Al Qamus*, kama ilivyotaja ile tafsiri ya kwanza pia na (4) vilivyotungwa na hata wasiokuwa Waislamu, kama *Al Munjid*, kama ilivyotaja ile tafsiri ya kwanza pia. Na wao Makadiyani wakawa na mdomo mpana wa kusema uwongo kuwa hiyo "Siyo" tafsiri ya tamko hilo! Wanatafuta hizaya makusudi; nayo inawafika.

Kwa ajili ya kule kule kukanusha kwao uweza wa Mwenyezi Mungu kuwafufua baadhi ya viumbe vyake papa hapa ulimwenguni (kisha akavifisha tena) kwa ajili ya kuonyesha miujiza yake, ndiyo Makadiyani wameipindua chini juu Aya hii walioifanya kuwa ya 260 wakasema; "Njozi hiyo . . .' Ati maneno hayo yote ni ndoto si kweli!

mkizisamehe deni zenu) mkazifanya sadaka, basi ni bora kwenu. Ikiwa mnajua haya (basi fanyeni).

281. Na iogopeni Siku ambayo mtarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, kisha viumbe wote watalipwa kwa ukamilifu yote waliyoyachuma; nao hawatadhulumiwa.

282. Enyi mlioamini! Mnapokopeshana deni kwa muda uliowekwa, basi iandikeni. Na mwandishi aandike baina yenu kwa uadilifu, wala mwandishi asikatae kuandika; kama alivyomfunza Mwenyezi Mungu hivyo; basi naandike. Na ayatamke (maneno hayo ya kuandikwa hivyo, mkopa) ambaye juu yake iko haki; naye amwogope Mwenyezi Mungu, Mola wake; wala asipunguze cho chote ndani yake. Na kama yule ambaye juu yake iko Haki (mkopaji) ni mpumbavu au mnyonge au yeye hawezi kuandikisha mwenyewe basi aandikishe msimamizi wake (yule mtu anayemwendeshea mambo yake) kwa uadilifu. Na mshuhudishe mashahidi wawili katika watu wenu wanaume (Waislamu). Lakini ikiwa hakuna wanaume wawili, basi mwanamume mmoja na wanawake wawili (watatosha); katika wale mnaowakubali kuwa mashahidi. Ili kama mmoja wao (katika wale wanawake) akipotea, mmoja wao amkumbushe mwingine. Na mashahidi wasikatae waitwapo. Wala msipuze kuiandika (hiyo deni), ikiwa ndogo au kubwa mpaka muda wake; hayo (ya kuandika) ndiyo bora mbele ya Mwenyezi Mungu, na imara zaidi kwa ushahidi, na pia ni ya kupelekea kuwa msiwe na shaka. Ila ikiwa ni biashara iliyohudhuria mnayopeana baina yenu, basi si vibaya kwenu msipoiandika. Na shuhudisheni mnapouziana. Wala asitiwe taabuni mwandishi wala shahidi. Na kama mkifanya hivyo; basi hakika hilo ni kosa kwenu. Na mwogopeni Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu anakuilimisheni; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

وَأَن تَصَدَّقُوا خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٨٠﴾
وَاتَّقُوا يَوْمًا تُرْجَعُونَ فِيهِ إِلَى اللَّهِ ثُمَّ تُوَفَّىٰ
كُلُّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٢٨١﴾
يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا تَدَايَنتُم بِدَيْنٍ إِلَىٰ
أَجَلٍ مُّسَمًّى فَاكْتُبُوهُ ۚ وَلْيَكْتُب بَّيْنَكُمْ كَاتِبٌ
بِالْعَدْلِ ۚ وَلَا يَأْبَ كَاتِبٌ أَن يَكْتُبَ كَمَا عَلَّمَهُ اللَّهُ
فَلْيَكْتُبْ ۚ وَلْيُمْلِلِ الَّذِي عَلَيْهِ الْحَقُّ وَلْيَتَّقِ اللَّهَ
رَبَّهُ وَلَا يَبْخَسْ مِنْهُ شَيْئًا ۚ فَإِن كَانَ الَّذِي عَلَيْهِ
الْحَقُّ سَفِيهًا أَوْ ضَعِيفًا أَوْ لَا يَسْتَطِيعُ أَن يُمِلَّ هُوَ
فَلْيُمْلِلْ وَلِيُّهُ بِالْعَدْلِ ۚ وَاسْتَشْهِدُوا شَهِيدَيْنِ
مِن رِّجَالِكُمْ ۖ فَإِن لَّمْ يَكُونَا رَجُلَيْنِ فَرَجُلٌ وَامْرَأَتَانِ
مِمَّن تَرْضَوْنَ مِنَ الشُّهَدَاءِ أَن تَضِلَّ إِحْدَاهُمَا
فَتُذَكِّرَ إِحْدَاهُمَا الْأُخْرَىٰ ۚ وَلَا يَأْبَ الشُّهَدَاءُ
إِذَا مَا دُعُوا ۚ وَلَا تَسْأَمُوا أَن تَكْتُبُوهُ صَغِيرًا أَوْ كَبِيرًا
إِلَىٰ أَجَلِهِ ۚ ذَٰلِكُمْ أَقْسَطُ عِندَ اللَّهِ وَأَقْوَمُ
لِلشَّهَادَةِ وَأَدْنَىٰ أَلَّا تَرْتَابُوا ۖ إِلَّا أَن تَكُونَ
تِجَارَةً حَاضِرَةً تُدِيرُونَهَا بَيْنَكُمْ فَلَيْسَ
عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَلَّا تَكْتُبُوهَا ۗ وَأَشْهِدُوا إِذَا تَبَايَعْتُمْ
وَلَا يُضَارَّ كَاتِبٌ وَلَا شَهِيدٌ ۚ وَإِن تَفْعَلُوا
فَإِنَّهُ فُسُوقٌ بِكُمْ ۗ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۖ وَيُعَلِّمُكُمُ اللَّهُ ۗ
وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٢٨٢﴾

---

Ukafiri mkubwa kweli kweli huu—kumpindulia Mwenyewe Mwenyezi Mungu maneno yake wakasema: "Kama ilivyoelezwa ndoto ya Nabii Yusuf." Kuko wapi kunasibishwa haya ya hakika (kimacho si katika ndoto) na ndoto ya Nabii Yusuf? Katika ndoto ya Nabii Yusuf, Mwenyewe Mwenyezi Mungu amesema *"Ruuyaa"* (Ndoto). Na akalikariri tamko hilo humo katika kisa cha Nabii Yusuf. Liko wapi — katika kisa hiki — tamko la *"Ruuyaa"*? Khatari kabisa watu hawa juu ya Waislamu na dini yao. Lakini Mwenyezi Mungu hatasimama nao Inshaallah.

261-267. Hizi zote ni Aya za kuhimiza kutoa katika njia za kheri na za kuonyesha fadhila anazowapa Mwenyezi Mungu kwa kufanya hayo; lakini kwa sharti wafanye (a) kwa ajili ya Mwenyezi Mungu — isiwe kuonyesha watu tu. Na wawe wanatoa (b) vilivyo vizuri. Wakitoa visivyokuwa vizuri hawatapata thawabu kubwa namna hiyo. Wala (c) isiwe kuwaudhi hao wanaowapa wala (d) kuwasumbulia. Ikiwa si hivyo basi hapana thawabu ila khasara tu. Na maneno mazuri yatakuwa bora kuliko sadaka hizo na (e) kwa sharti kiwe hicho unachokitoa cha halali yako.

283. Na kama mkiwa safarini na hamkupata mwandishi, basi (mdai) apewe (astakabadhishwe) (kitu kiwe) rahani mikononi mwake. Na kama mmoja wenu amewekewa amana na mwingine, basi aliyeaminiwa airudishe amana ya mwenzake, na amche Mwenyezi Mungu, Mola wake. Wala msifiche ushahidi (japo juu ya nafsi zenu). Na atakaeficha basi hakika moyo wake ni wenye kuingia dhambini. Na Mwenyezi Mungu huyajua (yote) mnayoyatenda.

وَإِن كُنتُمْ عَلَىٰ سَفَرٍ وَلَمْ تَجِدُوا كَاتِبًا فَرِهَٰنٌ
مَّقْبُوضَةٌ ۖ فَإِنْ أَمِنَ بَعْضُكُم بَعْضًا فَلْيُؤَدِّ
الَّذِي اؤْتُمِنَ أَمَانَتَهُ وَلْيَتَّقِ اللَّهَ رَبَّهُ ۗ
وَلَا تَكْتُمُوا الشَّهَادَةَ ۚ وَمَن يَكْتُمْهَا فَإِنَّهُ آثِمٌ
قَلْبُهُ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ

284. (Vyote) vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini ni vya Mwenyezi Mungu. Na kama mkidhihirisha yaliyomo katika nyoyo zenu, au mkiyaficha, Mwenyezi Mungu atakutakeni hisabu ya (yote) hayo; kisha amsamehe amtakaye (kwa kuwa katubia) na amuadhibu amtakaye (kwa kuwa hakutubia). Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.

لِّلَّهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَإِن تُبْدُوا
مَا فِي أَنفُسِكُمْ أَوْ تُخْفُوهُ يُحَاسِبْكُم بِهِ اللَّهُ ۖ
فَيَغْفِرُ لِمَن يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَن يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ
كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٨٤﴾

285. Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake, na Waislamu, (pia wameamini hayo): wote wamemwamini Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume yake; (nao hao Waislamu na Mtume wao husema), "Hatutafautishi baina ya yo yote katika

آمَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِن رَّبِّهِ
وَالْمُؤْمِنُونَ ۚ كُلٌّ آمَنَ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ
وَرُسُلِهِ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِّن رُّسُلِهِ ۚ وَقَالُوا

---

268-271. Hapa Mwenyezi Mungu anawapa moyo mkubwa watoao kuwa Kila Wakitoa na Mungu atawazidishia; na anawahadharisha na kusikiliza wasiwasi wa Shetani anaoutia katika nyoyo zao kuwa 'Mkitoa Mtaishiwa.' Basi Mungu anawaambia 'Toeni tu wala Hamtaishiwa; bali mtatengenekewa duniani na Akhera.'

270. Nadhiri ya kusema 'Nikikipata kitu fulani nitafanya jambo fulani' au 'Akipona mtu wangu nitatoa. . . .' na kama hivi hili si jambo linalopendeza katika Sharia, japo kuwa watu wengi wanalifanya na wakaona wanafanya jambo lililosuniwa na Sharia; kumbe kinyume chake. Ni lenye kubeuliwa.

Hii inaitwa 'Nadhrul Mujaazaa'; ya kumlipa Mungu kwa kitendo atakachokufanyia. Unasema 'Akinifanyia langu hili na mimi lake nitamfanyia na kama hakunifanyia na mimi simfanyii'.

Basi Mtume KAIKATAZA Nadhiri hii na akasema kuwa Nadhiri hii haileti kheri ila ni sababu ya bakhili kutoa ambacho asingekitoa ila kwa kuwa yeye naye kupewa. Hadithi hii wameipokea Maimamu hawa: Al Bukhary, Muslim na wengine wote.

Na watu huzishughulikia Nadhiri hizi Kuziweka na Kuziondowa; zikaanguka nyali na visomo vya kuteua, (kuchagua) khasa Suratud Dahr, wakiona 'YUUFUUNA BINNADHRI' iliyomo katika Aya yake ya 7 ndivyo muradi hayo wanayoyafanya, Wala sivyo. Tazama muradi wake kwenye tafsiri yetu hii.

Nadhiri inayopendwa na sharia kuwa Mwenyezi Mungu kakufanyia unalolitaka ukafanya jambo la kheri kwa kumshukuru neema hiyo aliyokuteremshia; sio kuagana Naye mbele – Ukinifanyia Nitakufanyia.

Na juu ya hivi; Ukiweka Nadhiri namna hizi sharti utekeleze ulilolisema ili usikusanye mawili —

(a) Lisilokuwa ndilo na

(b) Kutotimiza waadi.

272. Hapa anaambiwa Mtume na kila mwamrisha mema na kukataza mabaya—kuwa lililo juu yao ni kufikisha hizo amri na makatazo. Wala hapana juu yao madhara yo yote kama hawatafuatwa. W'ao watapata thawabu zao za huko kuamrisha na kukataza japokuwa hawakusikilizwa.

273. Hapa wanabainishwa watu ambao ni bora kuwapa sadaka zako—wawe masikini kweli na wawe watu wa dini.

275. Hizi ni Aya za Kuharimisha Kukopesha kwa Riba. Mwenyezi Mungu amemuhadidi kweli kweli mlaji riba—amemwambia ajijuvye kuwa yumo katika vita baina yake yeye na Mwenyezi Mungu. Makamio makubwa

Mitume yake (wote tunawaamini)." Na husema: "Tumesikia na tumetii. (Tunakuomba) msamaha, Mola wetu! Na marejeo ni kwako."

286. Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yo yote ila yaliyo sawa na uweza wake. (Faida ya) yale iliyoyachuma (hiyo nafsi) ni yake na hasara ya yale iliyoyachuma ni juu yake. (Husema): "Mola wetu!

سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا غُفْرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ ﴿٢٨٥﴾

لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا لَهَا مَا كَسَبَتْ
وَعَلَيْهَا مَا اكْتَسَبَتْ رَبَّنَا لَا تُؤَاخِذْنَا إِنْ نَسِينَا
أَوْ أَخْطَأْنَا رَبَّنَا وَلَا تَحْمِلْ عَلَيْنَا إِصْرًا كَمَا

---

kabisa kama ya wale Maharamia Wezi wa kukatwa Mikono na Miguu yao, Wanaowashambulia Watu Wakawanyang'anya Chao na Wakawatoa Roho zao. Basi na Walaji Riba wamewekwa katika daraja hii. Na hapana shaka kuwa Walaji Riba wanakhasiri vya watu na wanatoa Roho zao.

Iliposemwa yamekwisha mthibitikia yale (mali) yaliyopita (aliyokwisha yapata) wamekusudiwa wale makafiri waliokuwa wakila Riba kabla ya kuja Sharia ya kuwabainishia kuwa hayo ni haramu. Basi wao wanaambiwa kuwa tangu sasa—baada kwisha kupata habari hii—wasipokee Riba kwa hizo mali wanazozidai. Wapokee kile kile walichokikopesha. Na Riba walizozila kabla ya hapo hawaambiwi wawarejeshee wenyewe. Lakini amesema Mwenyewe Mwenyezi Mungu kuwa amri yao huko Akhera iko mikononi Kwake (Mwenyezi Mungu) — anajua Mwenyewe ya kufanya. Na hukumu hii imetajwa tena katika Aya ya 278.

Ama mlaji Riba baada ya kuja dini ya Uislamu — anapotubia ili asalimike na hiyo adhabu kubwa kabisa ya Mwenyezi Mungu aliyowaekea Walaji Riba — inampasa awarejeshee wenyewe wote Riba yote ile aliyoichukua kwao — ajisazie kile kile chake tu alichowakopesha, pasina kuzidisha senti moja. Na kama wamekufa awape mawarithi wao. Na ikiwa hawana mawarithi wawatumilie mali yao hayo katika njia za kheri. Si 'yaliyopita yamekwisha kupita.'

Hukumu hii imebainishwa katika Aya ya 279.

280. Kama walivyoamrishwa wawakopeshe watu pasina riba ndivyo wanavyoamrishwa wawasitahamilie hao wanaowadai — japo muda ukifika-maadam wamo katika dhiki bado. Na wanashawikishwa wawasamehe khasa, wasiwadai maisha yao, hata baada ya kutengenekewa.

282. Hapa wanahimizwa watu waandikiane wanapokopeshana ili isiwe mzozo na kukanushiana baadaye-hata kikiwa kitu kidogo waandikiane pia.

Na hapo wanapokwenda kuandikiana awe yule aliyekopa ndiye msemaji wa maneno haya ya deni. Inachelewa asije akatamka yule mkopeshaji—akaongeza kitu—na huyo mkopa akaona haya kumrejeza kwani Uso Wa Kufadhiliwa Uchini. Na wanaambiwa wale wajuzi wa kuandika kuwa wasikatae kuwaandikia wale wasiojua kuandika. Watu ni Kufaana.

Na kama walivyoambiwa Waandike ndivyo wanavyoambiwa Washuhudishe vile vile — juu ya kuwa wameandika. Na wale mashahidi watie sahihi zao humo.

Na mashahidi sharti wawe wanaume wawili Waislamu. Wakikosekana wanaume basi kila mahala pa mwanamume mmoja iwe wanawake wawili, kwani hifdhi za wanawake ni ndogo kuliko za wanaume. Na wanaambiwa watu kuwa wasikatae kuwa mashahidi kwani kushuhudia ni jambo la kheri—jambo la kuthibitisha haki au kukanusha batili. Basi wajibu ifanywe.

Ama biashara ya kupeana mkono kwa mkono hiyo haishurutiziwi kuandikiana lakini iwekewe mashahidi.

Na ilipoambiwa 'Asitiwe taabuni mwandishi wala shahidi' ni kuonyesha kwamba ikiwa kazi hiyo ya kuandika au ya kwenda kushuhudiliwa itawachukulia muda mrefu hao mashahidi na hao waandishi na itawazuilia na kutafuta riziki yao ya wakati huo; basi wapewe ijara.

Makadiyani wamepotoa hapa kwenye hii Aya waliyosema kuwa ni ya 283 katika habari za mashahidi. Mwenyezi Mungu amesema *"Shahydayn Min Rijaalikum"* (Mashahidi wawili katika wanaume wenu) yaani Waislamu. Mpaka muwakose mashahidi walio Waislamu ndipo muweke mashahidi wasiokuwa Waislamu, kama ilivyo katika Aya ya 106 ya *Suratul Maida* na nyinginezo. Wao katika Aya hii ya *Suratul Baqarah* waliyoita ya 283 wameandika hivi: "yaani mashahidi wawe watu wenu wanaokaa mahali mlipo, wasiwe wageni ili wakitakiwa kutoa ushahidi watokee mara moja". Lakini walipofika Aya 106 ya *Suratul Maida* (waliyoifanya ya 107) walihizika wakakiri kuwa mashahidi sharti wawe Waislamu ila wakati wa kutompata Mwislamu kama katika safari. Lakini walijitia pambani wakaandika kuwa maneno hayo kayasema Kadhi maarufu, Shureh. La! Mambo haya hakuyasema Kadhi Shureh wala mwingineo; haya kayasema Mwenyewe Mwenyezi Mungu kama yalivyo hapo kwenye hiyo Aya ya 106 ya *Suratul Maida* na nyinginezo.

283. Na hapa inaambiwa kwamba watu wakiwa mahali ambapo hapana mwandishi na wamekopeshana, basi

Usitutese kama tukisahau (tukaacha yaliyo mema) au tukikosa (tukafanya mabaya). Mola wetu! Na usitubebeshe mzigo kama uliowabebesha wale waliokuwa kabla yetu. Mola wetu! Usitutwike tusiyoyaweza, na utusamehe, na utughufirie, na uturehemu. Wewe ndiye Mlinzi wetu. Basi tusaidie juu ya watu makafiri."

حَمَلْتَهُ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِنَا ۚ رَبَّنَا وَلَا تُحَمِّلْنَا مَا
لَا طَاقَةَ لَنَا بِهِ ۖ وَاعْفُ عَنَّا وَاغْفِرْ لَنَا وَارْحَمْنَا ۚ
أَنتَ مَوْلَانَا فَانصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٢٨٦﴾

---

yule aliyekopeshwa atowe kitu ampe yule aliyemkopesha kiwe amana (rahani) katika mkono wake. Atakapompa haki yake na yeye atamrejeshea kitu chake. Na akishindwa kumpa kitauzwa na hakimu alipwe yeye mdai haki yake, na kinachosalia apewe mwenyewe aliyekuwa akidaiwa.

Hii ndiyo faida ya kupokea rahani katika Uislamu—kuwa anaposhindwa kulipa kinauzwa kitu kile na Serikali, analipwa haki yake huyo anayedai, na kinachosalia anarejeshewa mwenyewe. Sio ukitimia muda iwe mdai (mwenye deni) kukifilisi chote wala si kuwa yeye mdai—katika muda wa deni—anatumia ghila yake kitu hicho kilichowekwa rahani. Hiyo ni riba, siyo rahani iliyokubalishwa katika Sharia.

285. Hizi Aya mbili za *Amanar Rasul*—Aya ya 285 na 286—ni Aya zenye fadhila kubwa kabisa kama ile *Ayatul Kursiy* 255. Na imehimizwa kusomwa mwahala mle mlimosuniwa kusomwa ile *Ayatul Kursiy*.

Aya hizi 2 zinaonyesha baadhi ya sifa za Waislamu na mambo yao wanayoyaamini. Na moja katika hayo ni kuwa wanawakubali Mitume wote wa Mwenyezi Mungu waliokuwa KABLA ya Nabii Muhammad. Quran yote inasema *'minqablika'* yaani waliokuwa kabla yako.

Kama alivyobainisha hivi Mwenyezi Mungu katika Quran yote—kuwa Mitume wote walipewa Utume kabla ya Nabii Muhammad. Yeye Nabii Muhammad ndiye wa Mwisho—*Khaatamaan Nabiyyin*. Asiyesadiki hivi akamsadiki anayejisingizia kuwa kapewa Utume Baada ya Nabii Muhammad basi mtu huyo ni kafiri pamoja na huyo mtume wake. Waislamu hawamkatai hata mmoja katika Watume (Mitume) waliokuwa kabla ya Nabii Muhammad, ila wanaitakidi kuwa Sharia zao za mambo ya Kufanya sasa hazifuatwi. Hizi ni zama za kufuata Sharia aliyokuja nayo Nabii Muhammad katika mambo ya Kufanya. Ama katika mambo ya Itikadi Mitume wote wamekuja na Sharia namna moja, kama alivyosema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 13 ya *Suratish Shura* (na katika Sura nyenginezo).

Na Aya hizi za 285 na 286 zinafundisha vile vile baadhi ya Adabu za Uislamu na Dua za kuomba. Na ni za Kutaja fadhila za Mwenyezi Mungu zilizoko juu ya waja Wake — kuwa Hawakalifishi wasiyoyaweza, bali hata 'Magumu sana' tu hawakalifishi. Anawakalifisha yaliyo mepesi kwao. Wala hawatesi wanapofanya jambo kwa kusahau au kwa Dharura kubwa. Na kuonyesha vile vile kuwa mzee hatateswa kwa kosa la mtoto wala mtoto hatateswa kwa kosa la mzee wala . . . kwa kosa la . . . Kila mtu ana lawama za amali zake mwenyewe—si za mtu mwengine. Lakini juu yake kuamrisha mema na kukataza mabaya—si juu yake wakitofuata.

Soma kwa urefu habari ya mwanaharamu katika maelezo ya Aya ya 15 ya Bani Israel.

آياتها ٢٠٠ (٣) سُورَةُ آلِ عِمْرَانَ مَدَنِيَّة (٨٩) رُكُوعَاتُهَا ٢٠

*Ina Aya 200* *Ina Makara 20*

# SURAT AALI IMRAN

*(Imeteremka Madina)*

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

1. Alif Lam Mym.

2. Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye — Mwenye uhai wa milele, na Mwendeshaji wa mambo yote.

3. Amekuteremshia Kitabu kwa haki, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake. Na aliteremsha Taurati na Injili.

4. Zamani — ziwe uwongozi kwa watu. Na akateremsha vitabu vyengine vya kupambanua baina ya haki na batili. Hakika wale waliozikufuru Aya za Mwenyezi Mungu watakuwa na adhabu kali; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye kulipa.

5. Bila shaka Mwenyezi Mungu Kwake hakifichiki cho chote kilichomo ardhini wala kilichomo mbinguni.

6. Yeye ndiye anayekutengenezeni sura matumboni jinsi apendavyo. Hakuna aabudiwaye ila yeye, Mwenye nguvu na Mwenye hikima.

7. Yeye ndiye aliyekuteremshia Kitabu (hiki Quran). Ndani yake zimo Aya *Muhkam* (nyepesi kufahamika) ambazo ndizo msingi (asili) wa Kitabu (hiki). Na ziko nyingine *Mutashaabihat* (zinababaisha, kama habari za Akhera, za Peponi na Motoni na mengineyo ambayo yamekhusika na Roho). Wale ambao nyoyoni mwao mna upotofu wanafuata zile zinazobabaisha kwa kutaka kuwaharibu watu na kutaka kujua hakika yake vipi. na hakuna ajuaye hakika yake vipi; ila Mwenyezi Mungu. Na wale waliozama katika ilimu husema: "Tumeziamini, zote zimetoka kwa Mola wetu." Na hawakumbuki isipokuwa wenye akili.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

الٓمٓ (١)
اللَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ (٢)
نَزَّلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ
يَدَيْهِ وَأَنْزَلَ التَّوْرَاةَ وَالْإِنْجِيلَ (٣)
مِنْ قَبْلُ هُدًى لِلنَّاسِ وَأَنْزَلَ الْفُرْقَانَ ۗ
إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِ اللَّهِ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ ۗ
وَاللَّهُ عَزِيزٌ ذُو انْتِقَامٍ (٤)
إِنَّ اللَّهَ لَا يَخْفَىٰ عَلَيْهِ شَيْءٌ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي
السَّمَاءِ (٥)
هُوَ الَّذِي يُصَوِّرُكُمْ فِي الْأَرْحَامِ كَيْفَ يَشَاءُ ۚ
لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ (٦)
هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ مِنْهُ آيَاتٌ
مُحْكَمَاتٌ هُنَّ أُمُّ الْكِتَابِ وَأُخَرُ مُتَشَابِهَاتٌ ۖ
فَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ زَيْغٌ فَيَتَّبِعُونَ مَا تَشَابَهَ
مِنْهُ ابْتِغَاءَ الْفِتْنَةِ وَابْتِغَاءَ تَأْوِيلِهِ ۗ وَمَا يَعْلَمُ
تَأْوِيلَهُ إِلَّا اللَّهُ ۗ وَالرَّاسِخُونَ فِي الْعِلْمِ
يَقُولُونَ آمَنَّا بِهِ كُلٌّ مِنْ عِنْدِ رَبِّنَا ۗ وَمَا يَذَّكَّرُ إِلَّا
أُولُو الْأَلْبَابِ (٧)

---

1. Tumekwishabainisha muradi wake katika mwanzo wa *Suratil Baqarah.*

2. Majina mawili haya '*Alhayyul Qayyum*' katika majina makubwa kabisa katika Majina ya Mwenyezi Mungu.

3. Iliposemwa 'Kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake' ni kuonyesha — kama vile tulivyobainisha katika Aya ya 285 ya *Suratil Baqarah* — kuwa 'Katika mambo ya Itikadi Mitume wote wamekuja na Dini moja.'

7. Basi watu wasijitatize kwa hizo Aya chache *Mutashaabihat.*

8. (Hao wenye akili husema) "Mola wetu! Usizipotoe nyoyo zetu baada ya kutuongoza, na utupe rehema itokayo kwako; hakika Wewe ndiwe Mpaji mkuu."

رَبَّنَا لَا تُزِغْ قُلُوبَنَا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا وَهَبْ
لَنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً ۚ إِنَّكَ أَنتَ الْوَهَّابُ ﴿٨﴾

9. "Mola wetu! Wewe ndiwe Mkusanyaji wa watu katika Siku isiyo na shaka ndani yake. Hakika Mwenyezi Mungu havunji miadi."

رَبَّنَا إِنَّكَ جَامِعُ النَّاسِ لِيَوْمٍ لَّا رَيْبَ فِيهِ ۚ
إِنَّ اللَّهَ لَا يُخْلِفُ الْمِيعَادَ ﴿٩﴾

10. Kwa hakika wale waliokufuru, mali zao hazitawafaa wala watoto wao hata kidigo kwa Mwenyezi Mungu; na hao (watakuwa) kuni za Moto

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَن تُغْنِيَ عَنْهُمْ أَمْوَالُهُمْ وَلَا
أَوْلَادُهُم مِّنَ اللَّهِ شَيْئًا ۖ وَأُولَٰئِكَ هُمْ
وَقُودُ النَّارِ ﴿١٠﴾

11. (Mwendo wa hawa makafiri wa uma wako Nabii Muhammad, ni) sawa na mwendo wa watu wa Firauni na wale waliokuwa kabla yao. Walikadhibisha Aya zetu. Kwa hivyo Mwenyezi Mungu aliwatia adabu kwa sababu ya madhambi yao; na Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.

كَدَأْبِ آلِ فِرْعَوْنَ وَالَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ ۚ
كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا فَأَخَذَهُمُ اللَّهُ بِذُنُوبِهِمْ ۗ وَاللَّهُ
شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿١١﴾

12. Waambie wale waliokufuru: "Karibuni hivi mtashindwa na mtakusanywa mtiwe kwenye Jahannam; nacho ni kikao kibaya kabisa."

قُل لِّلَّذِينَ كَفَرُوا سَتُغْلَبُونَ وَتُحْشَرُونَ إِلَىٰ
جَهَنَّمَ ۚ وَبِئْسَ الْمِهَادُ ﴿١٢﴾

13. Hakika imepatikana alama kubwa kwenu (nyinyi) katika yale makundi mawili yaliyokutana (Siku ya Vita vya Badr); kundi moja likipigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, na jingine makafiri. (Makafiri) wakawaona (Waislamu) zaidi kuliko wao mara mbili kwa kuona kwa macho; na Mwenyezi Mungu humtia nguvu, kwa nusra yake, amtakaye. Kwa yakini katika hayo yako mazingatio (makubwa) kwa wenye busara.

قَدْ كَانَ لَكُمْ آيَةٌ فِي فِئَتَيْنِ الْتَقَتَا ۖ فِئَةٌ
تُقَاتِلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَأُخْرَىٰ كَافِرَةٌ يَرَوْنَهُم
مِّثْلَيْهِمْ رَأْيَ الْعَيْنِ ۚ وَاللَّهُ يُؤَيِّدُ بِنَصْرِهِ
مَن يَشَاءُ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَعِبْرَةً
لِّأُولِي الْأَبْصَارِ ﴿١٣﴾

14. Watu wametiwa huba ya kupenda wanawake na watoto na mirundi ya dhahabu na fedha, na farasi wanaotunzwa vizuri, na wanyama na mashamba. Na hayo ni matumizi ya maisha ya katika dunia; na kwa Mwenyezi Mungu ndiko kwenye marejeo mazuri.

زُيِّنَ لِلنَّاسِ حُبُّ الشَّهَوَاتِ مِنَ النِّسَاءِ وَالْبَنِينَ
وَالْقَنَاطِيرِ الْمُقَنطَرَةِ مِنَ الذَّهَبِ وَالْفِضَّةِ
وَالْخَيْلِ الْمُسَوَّمَةِ وَالْأَنْعَامِ وَالْحَرْثِ ۗ ذَٰلِكَ
مَتَاعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۖ وَاللَّهُ عِندَهُ حُسْنُ الْمَآبِ ﴿١٤﴾

15. Sema: "Nikwambieni yaliyo bora kuliko hivyo?" Kwa ajili ya wamchao Mungu ziko bustani kwa Mola wao, zipitazo mito mbele yake. Watakaa humo milele na wake (zao) waliotakaswa (na kila uchafu na kila ubaya). Na wana radhi ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu anawaona (wote) waja (Wake).

قُلْ أَؤُنَبِّئُكُم بِخَيْرٍ مِّن ذَٰلِكُمْ ۚ لِلَّذِينَ
اتَّقَوْا عِندَ رَبِّهِمْ جَنَّاتٌ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا
الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا وَأَزْوَاجٌ مُّطَهَّرَةٌ وَرِضْوَانٌ
مِّنَ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِالْعِبَادِ ﴿١٥﴾

13. Siku ya vita vya Badr Waislamu walikuwa watu 300 hivi, wasiokuwa na silaha kamili. Na makafiri walikuwa watu 1000 waliojizatiti barabara. Lakini walipokuja kukabiliana, Mwenyezi Mungu aliwafanyisha wengi wale Waislamu katika macho ya makafiri. Makafiri wakawaona kuwa ni watu 2000; (yaani mara mbili kuliko wao), na hali ya kuwa ni 300 tu. Basi wakafanya woga nao makafiri na wakashindwa kwa ajili ya huo woga na mengineyo.

16. Ambao wanasema: "Mola wetu! Hakika sisi tumeamini, basi tughufirie madhambi yetu, na tuepushe na adhabu ya moto."

الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا إِنَّنَا آمَنَّا فَاغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا
وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿١٦﴾

17. Wafanyao subira, na wasemao kweli, na wanaotii, na watoao (sadaka), na waombao maghufira saa za kabla ya alfajiri.

الصَّابِرِينَ وَالصَّادِقِينَ وَالْقَانِتِينَ وَالْمُنفِقِينَ
وَالْمُسْتَغْفِرِينَ بِالْأَسْحَارِ ﴿١٧﴾

18. Mwenyezi Mungu ameshuhudia ya kwamba hakuna aabudiwaye kwa haki ila Yeye tu. Na Malaika na wenye ilimu, (wote wameshuhudia hayo); (Yeye) ndiye Mwenye kusimamisha uadilifu. Hakuna aabudiwaye kwa haki isipikuwa Yeye, Mwenye nguvu na Mwenye hikima.

شَهِدَ اللَّهُ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ وَالْمَلَائِكَةُ
وَأُولُو الْعِلْمِ قَائِمًا بِالْقِسْطِ ۚ لَا إِلَٰهَ إِلَّا
هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٨﴾

19. Bila shaka dini (ya haki) mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu. Na waliopewa Kitabu (Mayahudi na Manasara) hawakukhitalifiana ila baada ya kuwajia ilimu. (Walikhitalifiana) kwa sababu ya uhasidi uliokuwa baina yao. Na anayezikataa Aya za Mwenyezi Mungu (mara moja Mwenyezi Mungu atamuadhibu huko Akhera), na Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.

إِنَّ الدِّينَ عِندَ اللَّهِ الْإِسْلَامُ ۗ وَمَا اخْتَلَفَ الَّذِينَ
أُوتُوا الْكِتَابَ إِلَّا مِن بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْعِلْمُ
بَغْيًا بَيْنَهُمْ ۗ وَمَن يَكْفُرْ بِآيَاتِ اللَّهِ
فَإِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿١٩﴾

20. Na kama (makafiri) wakikuhoji, basi sema: "Nimeuelekeza uso wangu kwa Mwenyezi Mungu. Na walionifuata (wamefanya vivyo hivyo)." Na waambie wale waliopewa Kitabu na wale wasio na ilimu (makafiri wa Kiarabu na wengineo): "Je, mmejisalimisha (kwa Mungu)?" Kama wakijisalimisha wameongoka; na kama wakikengeuka, basi juu yako ni kufikisha tu. (Kama hawatafuata, lawama itawafika wenyewe). Na Mwenyezi Mungu anawaona (Mwenyewe) waja (Wake).

فَإِنْ حَاجُّوكَ فَقُلْ أَسْلَمْتُ وَجْهِيَ لِلَّهِ وَمَنِ
اتَّبَعَنِ ۗ وَقُل لِّلَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ وَالْأُمِّيِّينَ
أَأَسْلَمْتُمْ ۚ فَإِنْ أَسْلَمُوا فَقَدِ اهْتَدَوا ۖ وَّإِن
تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلَاغُ ۗ وَاللَّهُ
بَصِيرٌ بِالْعِبَادِ ﴿٢٠﴾

21. Wale wanaozikataa Aya za Mwenyezi Mungu, na wakawauwa Manabii pasipo haki, na wakawaua watu wanaoamrisha mambo ya haki, wapashe habari ya adhabu kali (inayowangoja).

إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَيَقْتُلُونَ
النَّبِيِّينَ بِغَيْرِ حَقٍّ وَيَقْتُلُونَ الَّذِينَ يَأْمُرُونَ
بِالْقِسْطِ مِنَ النَّاسِ فَبَشِّرْهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٢١﴾

22. Hao ndio ambao vitendo vyao vimeharibika katika dunia na Akhera. Nao hawatapata wasaidizi.

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ
وَمَا لَهُم مِّن نَّاصِرِينَ ﴿٢٢﴾

23. Huwaoni wale waliopewa (kufahamu) sehemu ya Kitabu (cha Mwenyezi Mungu. Mayahudi na Manasara) wanaitwa kukiendea Kitabu cha Mwenyezi Mungu ili kiwahukumu (haki) baina yao; kisha taifa moja miongoni mwao hukengeuka? Nao (daima) ni wenye kukengeuka tu.

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيبًا مِّنَ الْكِتَابِ
يُدْعَوْنَ إِلَىٰ كِتَابِ اللَّهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ يَتَوَلَّىٰ
فَرِيقٌ مِّنْهُمْ وَهُم مُّعْرِضُونَ ﴿٢٣﴾

16-17. Hapa Mwenyezi Mungu anataja baadhi ya sifa nzuri za kusifika Mwislamu mwema. Basi natusifike nazo.

24. Hayo (ya kutojali maamrisho ya Mwenyezi Mungu wala makatazo yake) ni kwa sababu walisema: "Hautatugusa Moto isipokuwa kwa siku chache;" na yakawadanganya katika dini yao yale waliyokuwa wakiyazua: (kuwa watasamehewa au watakaa siku chache tu Motoni).

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا لَن تَمَسَّنَا النَّارُ إِلَّا أَيَّامًا مَّعْدُودَاتٍ ۖ وَغَرَّهُمْ فِي دِينِهِم مَّا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٢٤﴾

25. Basi itakuwaje tutakapowakusanya Siku ambayo hapana shaka kuja kwake? Na kila nafsi italipwa kwa ukamilifu kila iliyochuma; nao hawatadhulumiwa.

فَكَيْفَ إِذَا جَمَعْنَاهُمْ لِيَوْمٍ لَّا رَيْبَ فِيهِ وَوُفِّيَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٢٥﴾

26. Sema (katika kumsifu Mwenyezi Mungu): "Ee Mola, uliyemiliki ufalme wote! Humpa ufalme umtakaye, na humwondolea ufalme umtakaye, na humtukuza umtakaye, na humdhalilisha umtakaye; kheri imo mkononi mwako. Bila shaka Wewe ni Mwenye uweza juu ya kila kitu."

قُلِ اللَّهُمَّ مَالِكَ الْمُلْكِ تُؤْتِي الْمُلْكَ مَن تَشَاءُ وَتَنزِعُ الْمُلْكَ مِمَّن تَشَاءُ وَتُعِزُّ مَن تَشَاءُ وَتُذِلُّ مَن تَشَاءُ ۖ بِيَدِكَ الْخَيْرُ ۖ إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٦﴾

27. "(Wewe) huuingiza usiku katika mchana (ukawa mchana mrefu siku za joto), na huuingiza mchana katika usiku (usiku ukawa mrefu siku za baridi), na hutoa aliye hai katika yule asiye na uhai, na hutoa mfu katika yule aliye hai; na humpa riziki umtakaye bila hisabu."

تُولِجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَتُولِجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ ۖ وَتُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَتُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ ۖ وَتَرْزُقُ مَن تَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٢٧﴾

28. Walioamini wasiwafanye makafiri kuwa wapenzi wao (wa kuwapa siri zao) badala ya (Waislamu wenziwao). Na atakayefanya hivyo, basi hatakuwa na cho chote mbele ya Mwenyezi Mungu. Ila (ikiwa mnafanya urafiki nao wa juu juu tu hivi) kwa ajili ya kujilinda na shari zao. Na Mwenyezi Mungu anakutahadharisheni na adhabu yake. Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu (ya nyote nyiye na wengineo).

لَّا يَتَّخِذِ الْمُؤْمِنُونَ الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ مِن دُونِ الْمُؤْمِنِينَ ۖ وَمَن يَفْعَلْ ذَٰلِكَ فَلَيْسَ مِنَ اللَّهِ فِي شَيْءٍ إِلَّا أَن تَتَّقُوا مِنْهُمْ تُقَاةً ۗ وَيُحَذِّرُكُمُ اللَّهُ نَفْسَهُ ۗ وَإِلَى اللَّهِ الْمَصِيرُ ﴿٢٨﴾

29. Sema: "Kama mkificha yaliyomo vifuani mwenu au mkiyadhihirisha (Mungu atakulipeni tu kwani) Mwenyezi Mungu anayajua; na anayajua yaliyomo mbinguni na yaliyomo ardhini; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.

قُلْ إِن تُخْفُوا مَا فِي صُدُورِكُمْ أَوْ تُبْدُوهُ يَعْلَمْهُ اللَّهُ ۗ وَيَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٩﴾

30. Siku ambayo kila nafsi itakuta mema iliyoyafanya yamehudhurishwa, na pia ubaya ilioufanya. Itapenda lau kungekuwa na masafa marefu baina ya ubaya huo na yeye. Na Mwenyezi Mungu anakutahadharisheni na adhabu yake. Na Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja (wake).

يَوْمَ تَجِدُ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ مِنْ خَيْرٍ مُّحْضَرًا وَمَا عَمِلَتْ مِن سُوءٍ تَوَدُّ لَوْ أَنَّ بَيْنَهَا وَبَيْنَهُ أَمَدًا بَعِيدًا ۗ وَيُحَذِّرُكُمُ اللَّهُ نَفْسَهُ ۗ وَاللَّهُ رَءُوفٌ بِالْعِبَادِ ﴿٣٠﴾

---

24. Na kuna katika Waislamu wanaoghurika kwa maneno yasiyokuwa sahihi wakafanya mabaya bila ya kujali kwa kuona kuwa watasamehewa tu kwa ajili ya hayo wanayoyaitakidi.

27. Kumtoa aliye hai katika aliyekufa . . . ni kama kutoa ndege katika yai au kutoa mimea katika mbegu au mtoto mwema kuzaliwa na mzee mbaya au mtoto mbaya kuzaliwa na mzee mwema.

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٣١﴾

31. Sema: "Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu, basi nifuateni; (hapo) Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakughufirieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye maghufira (na) Mwenye rehema."

قُلْ أَطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ ۖ فَإِن تَوَلَّوْا فَإِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْكَافِرِينَ ﴿٣٢﴾

32. Sema: "Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume (wake). Na kama mkikengeuka, (Mwenyezi Mungu atakutieni adabu), kwani Mwenyezi Mungu hawapendi makafiri.

إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَىٰ آدَمَ وَنُوحًا وَآلَ إِبْرَاهِيمَ وَآلَ عِمْرَانَ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٣٣﴾

33. Hakika Mwenyezi Mungu alimchagua Adamu na Nuhu na kizazi cha Ibrahimu na kizazi cha Imrani (Babaake Musa; na Imrani mwengine aliye baba yake Maryamu) juu ya walimwengu wote (wa zama zao)

ذُرِّيَّةً بَعْضُهَا مِن بَعْضٍ ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٣٤﴾

34. Ni kizazi cha wao kwa wao (hicho); na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia (na) Mwenye kujua.

إِذْ قَالَتِ امْرَأَتُ عِمْرَانَ رَبِّ إِنِّي نَذَرْتُ لَكَ مَا فِي بَطْنِي مُحَرَّرًا فَتَقَبَّلْ مِنِّي ۖ إِنَّكَ أَنتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٣٥﴾

35. (Kumbukeni) aliposema mke wa Imrani (baba yake Maryamu katika kumwomba Mola wake): "Mola wangu! Nimeweka nadhiri kwako aliyomo tumboni mwangu kuwa wakfu (wa kutumikia mambo ya dini); basi nikubalie. Bila shaka Wewe ndiye usikiaye na ujuaye."

فَلَمَّا وَضَعَتْهَا قَالَتْ رَبِّ إِنِّي وَضَعْتُهَا أُنثَىٰ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا وَضَعَتْ وَلَيْسَ الذَّكَرُ كَالْأُنثَىٰ ۖ وَإِنِّي سَمَّيْتُهَا مَرْيَمَ وَإِنِّي أُعِيذُهَا بِكَ وَذُرِّيَّتَهَا مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ ﴿٣٦﴾

36. Basi alipomzaa, alisema: "Mola wangu! Nimemzaa mwanamke" — na Mwenyezi Mungu anajua sana aliyemzaa — "Na mwanamume (niliyefikiri kuwa nitamzaa) si sawa na mwanamke (niliyemzaa). Na nimempa jina Maryamu (mtumishi wa Mungu). Nami namkinga kwako, yeye na kizazi chake, (uwalinde) na Shetani aliyebaidishwa na rehema yako."

فَتَقَبَّلَهَا رَبُّهَا بِقَبُولٍ حَسَنٍ وَأَنبَتَهَا نَبَاتًا

37. Basi Mola wake akampokea (yule mtoto) kwa kabuli njema na akamkuza kukua kwema, na akamfanya Zakaria awe mlezi wake. Kila mara

---

31. Basi mtu anayedai mapenzi ya Mwenyezi Mungu na hali ya kuwa hendi mwendo aliouleta Mtume wa kufanya mema na kuacha mabaya — mwongo.

34. Aya hii inaonyesha kuwa vizazi hivi vinahusiana. Na kuonyesha kuwa — mara nyingi — wema huzaa wema, kwa hivi kila anayetaka kuoa na aoe nyumba zilizo nzuri kwa mwendo wa dini, siha, ilimu, akili, uhodari na mengineyo.

35-36. Mke wake Bwana Imrani alipokuwa na mimba — akadhani kuwa atazaa mtoto mwanamume — aliweka nadhiri kumfanya mtoto huyo mtumishi wa msikiti wa Baytil Makdis na wa mambo mengine ya dini — asiwe na kazi nyengine ila hiyo.

Lakini ilikuwa bahati mbaya. Akamzaa mwanamke. Basi akadhihirisha huzuni yake kwa Mungu; kisha akamwombea dua huyo mwanawe awe mtoto wa kheri na azae vijana wa kheri. Na akamwita vile vile Mtumishi wa mambo ya Mungu.

Basi akawa Bibi Maryamu ni bibi wa kheri na akamzaa mtoto wa kheri. Naye ni Nabii Isa. Bibi Maryamu ni mwanamke mtukufu mno kabisa.

37. Bwana Imrani — baba yake huyu Bibi Maryamu — alikuwa bwana mkubwa katika hao mabwana

Zakaria alipoingia chumbani (kwake) alikuta vyakula pamoja naye (huyo Maryamu). Akasema; "Ewe Maryamu! Unapata wapi hivi?" Akasema: "Hivi vinatoka kwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila kuwaza (mwenyewe)."

حَسَنًا وَكَفَّلَهَا زَكَرِيَّا ۖ كُلَّمَا دَخَلَ عَلَيْهَا زَكَرِيَّا
الْمِحْرَابَ وَجَدَ عِندَهَا رِزْقًا ۖ قَالَ يَا مَرْيَمُ أَنَّىٰ
لَكِ هَٰذَا ۖ قَالَتْ هُوَ مِنْ عِندِ اللَّهِ ۖ إِنَّ اللَّهَ يَرْزُقُ
مَن يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٣٧﴾

38. Pale pale Zakaria akamwomba Mola wake, akasema: "Mola wangu! Nipe kutoka kwako mtoto mwema. Wewe ndiye usikiaye maombi (ya wanaokuomba)."

هُنَالِكَ دَعَا زَكَرِيَّا رَبَّهُ ۖ قَالَ رَبِّ هَبْ لِي مِن
لَّدُنكَ ذُرِّيَّةً طَيِّبَةً ۖ إِنَّكَ سَمِيعُ الدُّعَاءِ ﴿٣٨﴾

39. Mara Malaika wakamlingania, hali amesimama akisali chumbani, kwamba Mwenyezi Mungu anakupa khabari njema za (kuwa utazaa mtoto; umwite) Yahya, atakayekuwa mwenye kumsadikisha (Mtume atakayezaliwa) kwa neno litokalo kwa Mwenyezi Mungu (Naye ni Nabii Isa) na atakayekuwa bwana kabisa na mtawa na Nabii anayetokana na watu wema. (Nao ni nyinyi).

فَنَادَتْهُ الْمَلَائِكَةُ وَهُوَ قَائِمٌ يُصَلِّي فِي الْمِحْرَابِ
أَنَّ اللَّهَ يُبَشِّرُكَ بِيَحْيَىٰ مُصَدِّقًا بِكَلِمَةٍ
مِّنَ اللَّهِ وَسَيِّدًا وَحَصُورًا وَنَبِيًّا
مِّنَ الصَّالِحِينَ ﴿٣٩﴾

40. Akasema (Zakaria): "Mola wangu! Nitapataje mtoto, na hali uzee umenifikia, na mke wangu ni tasa?" Akasema (Mwenyezi Mungu): "Ndivyo vivyo hivyo; Mwenyezi Mungu hufanya apendavyo."

قَالَ رَبِّ أَنَّىٰ يَكُونُ لِي غُلَامٌ وَقَدْ بَلَغَنِيَ الْكِبَرُ
وَامْرَأَتِي عَاقِرٌ ۖ قَالَ كَذَٰلِكَ اللَّهُ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ ﴿٤٠﴾

41. Akasema: "Mola wangu! Niwekee alama (ya kunitambulisha kuwa mke wangu kishashika mimba nipate kufurahi upesi)." Akasema: "Alama yako ni kuwa hutaweza kusema na watu kwa siku tatu isipokuwa kwa ishara tu. Na umtaje Mola wako kwa wingi na umtukuze (kwa kusali) wakati wa jioni na asubuhi."

قَالَ رَبِّ اجْعَل لِّي آيَةً ۖ قَالَ آيَتُكَ أَلَّا
تُكَلِّمَ النَّاسَ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ إِلَّا رَمْزًا ۗ وَاذْكُر
رَّبَّكَ كَثِيرًا وَسَبِّحْ بِالْعَشِيِّ وَالْإِبْكَارِ ﴿٤١﴾ ع

42. Na (kumbuka) Malaika waliposema: "Ewe Maryamu! Kwa hakika Mwenyezi Mungu amekuchagua na kukutakasa na kukutukuza kuliko wanawake wa ulimwengu (wote)."

وَإِذْ قَالَتِ الْمَلَائِكَةُ يَا مَرْيَمُ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَاكِ
وَطَهَّرَكِ وَاصْطَفَاكِ عَلَىٰ نِسَاءِ الْعَالَمِينَ ﴿٤٢﴾

---

wakubwa wacha Mungu waliokuwa zama hizo. Na baada ya kumzaa tu mtoto wake huyu alikufa. Basi mabwana hao waliokuwa pamoja naye walishindaniana kumlea yule Maryamu.

Mwisho wake wakawafikiana wapige kura (bahati nasibu); itakayemwangukia ndiye amlee. Kura yenyewe ilikuwa ni hii: Kila mmoja katika wao aitumbukize kalamu yake ya mwanzi katika maji ya moto yalikuwako hapo. Basi ambaye kalamu yake haitaibuka ndiye atakayemlea. (Yametajwa haya katika Aya ya 44 ya Sura hii).

Basi Kura hiyo ikamwangukia Nabii Zakariyya — mume wa mama yake mdogo huyo Bibi Maryamu.

Mwenyezi Mungu akamwonyesha Nabii Zakariyya karama nyingi za kijana huyu. Moja katika hizo ni kumkuta na vyakula vya namna visivyopatikana kwa watu wengine; na anapomwuliza husema kuwa karuzukiwa na Mungu.

38. Nabii Zakariyya kuona karama zile aliona naye aombe afanyiwe muujiza wa kuzaa, hali ya kuwa kishapindukia siku za kuzaa, na mkewe pia kapindukia. Akamzaa Nabii Yahya.

42. Hapa zinatajwa khabari za Bibi Maryamu alipokwisha kuwa mtu mzima na namna alivyo-bashiriwa na Malaika kwa mambo matukufu hayo.

43. "Ewe Maryamu! Mnyenyekee Mola wako na usujudu na uiname (kusali) pamoja na wainamao."

يٰمَرْيَمُ اقْنُتِيْ لِرَبِّكِ وَاسْجُدِيْ وَارْكَعِيْ مَعَ
الرّٰكِعِيْنَ ﴿٤٣﴾

44. Hizi ni khabari za ghaibu tunazokufunulia; nawe hukuwa nao walipokuwa wakitupa kalamu zao ndani ya maji (kwa kura, wajue) nani wao atamlea Maryamu, na hukuwa nao walipokuwa wakishindana.

ذٰلِكَ مِنْ اَنْۢبَآءِ الْغَيْبِ نُوْحِيْهِ اِلَيْكَ ۚ وَمَا
كُنْتَ لَدَيْهِمْ اِذْ يُلْقُوْنَ اَقْلَامَهُمْ اَيُّهُمْ يَكْفُلُ
مَرْيَمَ ۖ وَمَا كُنْتَ لَدَيْهِمْ اِذْ يَخْتَصِمُوْنَ ﴿٤٤﴾

45. (Kumbukeni) waliposema Malaika: "Ewe Maryamu! Mwenyezi Mungu anakupa khabari njema za (kumzaa mtoto bila ya mume, bali kwa kutamkwa) neno tu litokalo kwake (la kukwambia 'Zaa' ukazaa pasina kuingiliwa). Jina lake ni Masih, Isa, mwana wa Maryamu, mwenye hishima katika dunia na Akhera, na miongoni mwa waliopelekwa mbele na Mwenyezi Mungu."

اِذْ قَالَتِ الْمَلٰٓئِكَةُ يٰمَرْيَمُ اِنَّ اللّٰهَ يُبَشِّرُكِ
بِكَلِمَةٍ مِّنْهُ ۖ اسْمُهُ الْمَسِيْحُ عِيْسَى ابْنُ
مَرْيَمَ وَجِيْهًا فِى الدُّنْيَا وَالْاٰخِرَةِ وَمِنَ
الْمُقَرَّبِيْنَ ﴿٤٥﴾

46. "Naye atazungumza na watu (maneno ya dini) katika utoto (wake) na katika utuuzima (wake,) na (atakuwa) katika watu wema (kabisa)."

وَيُكَلِّمُ النَّاسَ فِى الْمَهْدِ وَكَهْلًا وَّمِنَ
الصّٰلِحِيْنَ ﴿٤٦﴾

47. (Maryamu) akasema: "Mola wangu! Nitapataje mtoto, na hali mtu yo yote hakunigusa?" Akasema (Mola wake): "Ndivyo vivyo hivyo; Mwenyezi Mungu huumba anavyopenda: anapohukumu jambo, huliambia: 'Kuwa', (basi) likawa."

قَالَتْ رَبِّ اَنّٰى يَكُوْنُ لِيْ وَلَدٌ وَّلَمْ يَمْسَسْنِيْ
بَشَرٌ ۗ قَالَ كَذٰلِكِ اللّٰهُ يَخْلُقُ مَا يَشَآءُ ۗ اِذَا قَضٰٓى
اَمْرًا فَاِنَّمَا يَقُوْلُ لَهٗ كُنْ فَيَكُوْنُ ﴿٤٧﴾

48. "Na (Mwenyezi Mungu) atamfunza kuandika na kujua ilimu na (kujua) Taurati na Injili."

وَيُعَلِّمُهُ الْكِتٰبَ وَالْحِكْمَةَ وَالتَّوْرٰىةَ وَالْاِنْجِيْلَ ﴿٤٨﴾

49. "Na (atamfanya) Mtume kwa wana wa Israili, (kuwaambia): 'Nimekujieni na hoja kutoka kwa Mola wenu, ya kwamba nakuumbieni, katika udongo, kama sura ya ndege, kisha nampuliza, mara anakuwa ndege, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na ninawaponesha vipofu na wenye mabalanga, na

وَرَسُوْلًا اِلٰى بَنِيْٓ اِسْرَآءِيْلَ ەۙ اَنِّيْ قَدْ جِئْتُكُمْ
بِاٰيَةٍ مِّنْ رَّبِّكُمْ ۙ اَنِّيْٓ اَخْلُقُ لَكُمْ مِّنَ الطِّيْنِ
كَهَيْـَٔةِ الطَّيْرِ فَاَنْفُخُ فِيْهِ فَيَكُوْنُ طَيْرًا ۢ بِاِذْنِ
اللّٰهِ ۚ وَاُبْرِئُ الْاَكْمَهَ وَالْاَبْرَصَ وَاُحْيِ الْمَوْتٰى

---

44. Imekwishatajwa khabari hii katika maelezo ya Aya ya 37.

46. Tazama Makadiyani — kwa ushupavu wao wa kukataa miujiza — wanajitia kufuruni kwa kugeuza maneno ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu — baada ya kutaja kule kuzaliwa Nabii Isa kwa muujiza, bila ya baba, alitaja papo hapo kuwa saa hiyo hiyo alisema, kama yalivyo dhahiri haya tangu Aya ya 23 ya *Surat Maryam* mpaka Aya ya 33, ambayo ndiyo haya haya yaliyomo katika Aya hizi za *Surat Aali Imran*. "Fil Mahd" (yumo bado katika kitanda anacholaziwa mtoto); wao Makadiyani wamesema: "Neno la 'Mahdi' tumelifasiri hapa 'utoto' kwa kufuata mradi wake." Tena wakasema: "Yesu kusema maneno ya busara bado angali mtoto hakuna kioja cho chote ndani yake. Watoto wengi wenye akili na waliolelewa vizuri huzungumza namna hiyo." Tazama upotezi wa Makadiyani wanavyoigeuza 'Siku ya kuzaliwa' wakafanya ni wakati wa utoto ambao watoto wote wenye akili wakati huo wanaweza kusema maneno ya akili. Wanayapeperusha kusudi maneno ya Quran yaliyo dhahiri shahir, bila ya kumwogopa Muumba wala kuwastahi waumbwa. Ama kweli hawa makumbakumba.

49. Hapa inatajwa baadhi ya miujiza aliyokuja nayo Nabii Isa.

Katika mwisho wa maelezo ya Aya waliofanya kuwa ni ya 50 ya *Surat Aali Imran* anayotaja ndani yake Mwenyezi Mungu miujiza ya Nabii Isa kuwa aliwaambia watu wake ". . . nakuumbieni katika udongo kama sura ya ndege, kisha nampuliza, mara anakuwa ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu." Na wao Makadiyani

ninawafufua (baadhi ya) waliokufa, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, na nitakwambieni mtakavyovila na mtakavyoweka akiba katika nyumba zenu. Bila shaka katika haya imo hoja kwenu ikiwa nyinyi ni watu wa kuamini'!"

50. "Na (nitakuwa) msadikishaji wa yale yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati; na (nimekuja) ili nikuhalalishieni baadhi ya yale mliyoharimishiwa, na nimekujieni na hoja kutoka kwa Mola wenu. Kwa hivyo mcheni Mwenyezi Mungu na nitiini."

51. "Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu na ni Mola wenu. Basi mwabuduni. Hii ndiyo njia iliyonyoka."

بِإِذْنِ اللَّهِ ۖ وَأُنَبِّئُكُم بِمَا تَأْكُلُونَ وَمَا تَدَّخِرُونَ فِي بُيُوتِكُمْ ۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً لَّكُمْ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴿٤٩﴾

وَمُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ التَّوْرَاةِ وَلِأُحِلَّ لَكُم بَعْضَ الَّذِي حُرِّمَ عَلَيْكُمْ ۚ وَجِئْتُكُم بِآيَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُونِ ﴿٥٠﴾

إِنَّ اللَّهَ رَبِّي وَرَبُّكُمْ فَاعْبُدُوهُ ۗ هَٰذَا صِرَاطٌ مُّسْتَقِيمٌ ﴿٥١﴾

---

wameifasiri hivi: "nawaumbieni katika udongo sawa na matengenezo ya ndege, kisha napulizia ndani yake, mara huwa ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu." Na Aya hii imekaririwa mara mbili katika Qurani. Imetajwa katika Aya ya 49 ya *Surat Aali Imran* na Aya ya 110 ya *Suratul Maida*.

Lakini kwa ajili ya ukafiri wao Makadiyani wa kuikataa miujiza anayoitaja Mwenyezi Mungu Mwenyewe katika Quran, wamegeuza maana ya (1) Aya hii wakasema katika sahifa 107 mstari wa 21: "Hapa ustadi wa Nabii Isa wa kusema maneno kwa mifano unadhihirika vizuri. Kwanza anawafananisha wanafunzi wake na udongo — yaani watu wanyonge walio duni. Kisha kwa mafundisho yake anawatengeneza mara wanakuwa kama wafu waliotiwa roho zenye nguvu: na badala ya kutembea ardhini maisha ya kiduniani, wanakuwa kama ndege wapaao mbinguni." Tazama ukafiri wa Kikadiyani huu wa kupindua maneno ya Mungu. Khalafu wakajidai kutaja Aya za Quran za kuonyesha kuwa kuumba kunakhusika na Mungu tu. Na sisi tunawaambia vile vile: "Nakuhuisha kumekhusika na Mungu pia; na juu ya hivi alimpa Nabii Isa kwa idhini yake muujiza wa kuhuisha (wafu) watu wawili watatu kama alivyotwambia Mwenyewe Mwenyezi Mungu."

Na wamegeuza vile vile muradi wa (II) *"Waubriul Akmaha wal Abrasa"* (Na ninawaponesha vipofu na wenye mabalanga), Wao Makadiyani wamefasiri: "Na ninamponya kipofu na mwenye ukoma." Lakini katika maelezo — kwa ajili ya ule ukafiri wao wa kukataa miujiza aliyoitaja Mwenyezi Mungu katika hii Quran yake — wamegeuza wamesema: "Kama ujuavyo Manabii ni madaktari wakubwa wa roho. Kazi yao ni ngumu. Kumponya ambaye macho ya roho yake yamepofuka, na aliyeenewa na ukoma wa roho, ni kazi ngumu kupita kiasi." Enyi Makadiyani! Ikiwa Mitume yote ni Madaktari wakubwa wa roho — nao ndiyo kweli — kwa nini hapa akakhusishwa Nabii Isa kuwa anaponesha vipofu na wenye mabalanga? Ukafiri wenu mkubwa Makadiyani kwa kupotoa miradi (wingi wa muradi) ya Mwenyezi Mungu na dini yake; bali hata maana ya maneno yake. 'Abras' ni mwenye mabalanga. Wao — kusudi — wamefasiri "Mwenye ukoma" ili wapate fursa sahili zaidi ya kupindua muradi wa Mwenyezi Mungu. Shetani kawapa kazi kubwa kweli kweli — kujipania kwa mwisho wa jitihada yao kuharibu dini ya Mwenyezi Mungu. Na huku (a) kuponesha vipofu na wenye mabalanga amekukariri Mwenyezi Mungu kama alivyokariri kule (b) kufanya kwake Nabii Isa ndege wakaruka na (c) kuwahuisha baadhi ya wafu, kisha wakafa pale pale.

Na kama hawa Makadiyani walivyompinga Mwenyezi Mungu wakamkanushia ile miujiza miwili (a) na (b), ndivyo walivyompinga Mwenyezi Mungu vile vile wakamkanushia muujiza (c) alioutaja Mwenyewe Mwenyezi Mungu katika hii Quran yake! Wakasema "Hata hivyo Manabii wa Mwenyezi Mungu wanawahuisha wafu hao wa kiroho pia." Na hii habari ya kufufuka tumeijibu katika Aya ya 56 ya *Suratul Baqarah*. Hapana haja kusema tena. Rejelea tuliyoyaandika huko, na penginepo pia tumetaja. Makadiyani wanajitia pambani kusudi. Wanajua kuwa hapa inatajwa miujiza ya Nabii Isa kama — katika Aya nyingine na Sura nyingine — ilivyotajwa miujiza ya Mitume wengine: kama moto kwa Nabii Ibrahimu; chuma na majabali na ndege kwa Nabii Daudi; upepo na Majini na mengineyo kwa Nabii Suleimani; fimbo na mkono na mingineyo kwa Nabii Musa; na mengine kwa Mitume wengineo. Wanayajua haya Makadiyani, lakini — basi tu — wanajitia pambani, ili wafanikiwe katika kazi yao waliyopewa na kipenzi chao — shetani! Kwa hivyo wanafanya kila ushetani, wawaharibu vipenzi vya Rahmani.

Wanajibabaisha Makadiyani makusudi katika hiyo sahifa 107 na 108 kwa kutaja Hadithi ya baba yake Jabir. Wanajua kwa yakini kuwa kufufuliwa huku kulikotajwa hapa ni kufufuliwa kwa muda makhsusi tu, na kule kufufuliwa kulikotajwa katika Hadithi ya Jabir ni kufufuliwa kwa uhai huu wa dasturi. Wanajua SANA haya Makadiyani lakini wanataka tu SANA kuwapoteza SANA Waislamu.

52. Lakini Isa alipoona ukaidi wao (umeshitadi) alisema: "Nani watakuwa wasaidizi wangu kwendea (katika kuitangaza dini ya) Mwenyezi Mungu?" Wanafunzi (wake) wakasema: "Sisi ni wasaidizi wa (kutangaza dini ya) Mwenyezi Mungu. Tumemwamini Mwenyezi Mungu na ushuhudie kwamba sisi tumejisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu)."

فَلَمَّآ أَحَسَّ عِيسَىٰ مِنْهُمُ ٱلْكُفْرَ قَالَ مَنْ أَنصَارِىٓ إِلَى ٱللَّهِ ۖ قَالَ ٱلْحَوَارِيُّونَ نَحْنُ أَنصَارُ ٱللَّهِ ءَامَنَّا بِٱللَّهِ وَٱشْهَدْ بِأَنَّا مُسْلِمُونَ ﴿٥٢﴾

53. "Mola wetu! Tumeyaamini uliyoyateremsha, na tumemfuata Mtume, basi tuandike pamoja na washuhudiao."

رَبَّنَآ ءَامَنَّا بِمَآ أَنزَلْتَ وَٱتَّبَعْنَا ٱلرَّسُولَ فَٱكْتُبْنَا مَعَ ٱلشَّٰهِدِينَ ﴿٥٣﴾

54. Na (Mayahudi) walifanya hila; na Mwenyezi Mungu akazipindua hila zao; na Mwenyezi Mungu ndiye bora wa kupindua hila (za watu wabaya).

وَمَكَرُوا۟ وَمَكَرَ ٱللَّهُ ۖ وَٱللَّهُ خَيْرُ ٱلْمَٰكِرِينَ ﴿٥٤﴾

55. (Kumbukeni) Mwenyezi Mungu aliposema: "Ewe Isa! Mimi nitakutimizia muda wako wa kuishi (hawatakuuua hao maadui). Na nitakuleta kwangu, na nitakutakasa na wale waliokufuru, (hawataweza kukudhuru) na nitawaweka wale waliokufuata, juu ya wale waliokufuru, mpaka siku ya Kiyama. Kisha marejeo yenu yatakuwa kwangu, nikuhukumuni katika yale mliyokuwa mkikhitalifiana.

إِذْ قَالَ ٱللَّهُ يَٰعِيسَىٰٓ إِنِّى مُتَوَفِّيكَ وَرَافِعُكَ إِلَىَّ وَمُطَهِّرُكَ مِنَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ وَجَاعِلُ ٱلَّذِينَ ٱتَّبَعُوكَ فَوْقَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوٓا۟ إِلَىٰ يَوْمِ ٱلْقِيَٰمَةِ ۖ ثُمَّ إِلَىَّ مَرْجِعُكُمْ فَأَحْكُمُ بَيْنَكُمْ فِيمَا كُنتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٥٥﴾

---

54. Hii ni Aya moja katika Aya wanazopotezea watu hao Makadiyani na kutaka kuwagombanisha Waislamu wa kweli wenyewe kwa wenyewe. Tusiwasikilize kwa lolote lao wapotezi hao Makadiyani.

Makadiyani wamedhihirisha ukafiri wao barabara katika Aya hii ya *Aali Imran* walioifanya kuwa ni ya 55. Wamesema katika maelezo yake "Hila ya Mayuhudi ilipinduliwa na hila ya Mwenyezi Mungu ikashinda. Nabii Isa asife msalabani, akateremshwa hali ya kuzimia. Na baadaye akazindukana akaenda kufa, kifo cha ajali, hali ya mtu mzima mwenye miaka mingi, huko Kashmir." Tazama ukafiri wa Makadiyani na kumpinga Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu amesema katika Quran katika Aya ya *Suratun Nisaa* (katika Juzuu ya Sita = *Laa Yuhibbu*): *"Wamaa qataluuhu"* (Hawakumwua); *"Wamaa Salabuuhu"* (Wala hawakumsulubu). Wao wanamsuta Mwenyezi Mungu wanamwambia "Wamemsulubu, lakini hakufa msalabani Alitolewa yu hai akaenda akaishi Kashmiri." (Bara Hindi kwa Makadiyani)! Huu ukafiri dhahiri hauna hata pazia jepesi la kujisitiria. Basi natutahadhari na kusadiki ukafiri huo kuwa Nabii Isa kasulubiwa. Wala hakuna kabisa katika kitabu cho chote cha tafsiri ya Quran kabla ya Makadiyani kuwa Nabii Isa alikaa Kashmiri au Bara Hindi yo yote na akafa huko. Wamefanya Makadiyani haya ili wakimbie ule muujiza wa kuwa Nabii Isa kapandishwa mbinguni uliotajwa katika Quran katika Aya ya 157 ya *Suratun Nisaa* hiyo waliyoitaja kwa kusema: Pia tazama Sura 4:158. Hapo katika Juzuu ya 6 tukijaaliwa ndipo tutakapozidi kuona ukafiri wao wa kumsusuwika Mwenyezi Mungu. Mungu amesema hapo kuwa Hawakumsulubu . . . bali alimnyanyua (alimuinua) kwake. Wao wamesema: Kasulubiwa mpaka akazimia juu ya msalaba, kisha akatolewa akenda kuishi Kashmiri mpaka akafa huko kifo cha dasturi! Makadiyani wakiwa wanathubutu kumsuta Mungu, kitawashinda nini kuwasuta watu. Lakini moto unawangoja. *Hasbuhum Jahannam* — Unawatosha Moto wa Jahannam kuwatia adhabu wanayostahili (wanayostahiki). Ama wana kani ya kupoteza kweli kweli! Loo!

55. Uadui wa Makadiyani juu ya Uislamu unadhihiri hapa pia katika Aya waliyoita ya 56. Wao — kama baadhi chache kabisa ya Waislamu — wanasema "kuwa Nabii Isa hakupelekwa mbinguni yu hai, na maana ya — "Nitakuinua kwangu Nitakutukuza." Khiari yao wenyewe wakifasiri hivi au vinginevyo na wakisibu au wasisibu, Mwenyezi Mungu mwenyewe atawalipa kwa jitahada zao.

Tunayoyapinga sisi kwa Makadiyani ni kule kuwasingizia uwongo wanavyuoni kama vile wanavyomsingizia uwongo Mwenyezi Mungu na Mtumewe; bila ya kujali. Na kumsingizia uwongo Mwenyezi Mungu na Mtumewe na wanavvuoni kwa wasiyoyasema ni ukafiri mkubwa, nao ndio huu walio nao Makadiyani. Wao — badala ya

kusema "Sisi tunasema hivi" — wanasema "Mwenyezi Mungu katika Quran kasema hivi" na "Mtume katika Hadithi fulani, iliyo katika kitabu fulani kasema hivi" na "Mwanachuoni fulani ktika kitabu fulani kasema hivi"; na hali ya kuwa uwongo kabisa, na tamaa yao ni kuwa hayo matabu makubwa makubwa wanayoyataja, watu wa humu hawanayo.

Hapa wao wanataka kuwababaisha watu kuwa mwanachuoni mkubwa kabisa wa lugha ya Kiarabu na tafsiri ya *Quran* — *Az Zamakhshary* — anasema, kama wao, kuwa Nabii Isa hakupandishwa mbinguni, na kuwa ameyasema haya katika kitabu chake cha tafsiri kinachoitwa *Al Kashshaaf*. Na hali kuwa uwongo kabisa. Hapo penye "Mutawaffyka" (nitakutimizia muda wako wa kuishi) linafuatia ubavuni mwake tamko la "*Waraafiuka Ilayya*" (Na nitakuleta kwangu, — katika tamko hili ameandika *Az Zamakhashary* katika hii *Al Kashshaaf* yake: *Waraafiuka Ilayya Illaa Samaaiy wamaqarri Malaaikaty* (Nitakuleta kwangu kwenye mbingu zangu na mahala wanapokaa Malaika wangu). Na kitabu cha *Kashshaaf* kiko ulimwenguni, na humu mwetu pia kiko kwa baadhi ya wanavyuoni. Naitazamwe humo uzidi kuonekana uzandiki wa Makadiyani. Na vivi hivi ndivyo alivyoandika mfasiri wa kisasa kidogo Al Allaamatul Alusy; kinyume cha uwongo wao wanaomsingizia hapa Alusy kuwa anasema kama wao kuwa Nabii Isa hakupelekwa mbinguni.

Na kupelekwa Nabii Isa mbinguni kwa roho yake na kiwiliwili au kutopelekwa, haimo katika Arkanil Iyman wala katika Arkanil Isiam, lakini wao wanashikilia ili wamfanye huyo Ghulam Ahmad wao ndiye Al Masihu Isa. Basi nawaseme wenyewe watakavyo; ila wasiwasingizie tu wanavyuoni au Mtume au Mwenyezi Mungu wasiyoyasema.

Na huko kusema kwao kuwa "Bwana fulani kafasiri (*Mutawaffyka*) Nitakufisha", hakuna anayekataa akasema kuwa Nabii Isa hatakufa. Basi bure tu kutia chungu ya maneno na chungu ya majina ya wanavyuoni ambao wengi katika hao hawakutajwa kabisa katika — vitabu wanavyovitaja kama tulivyoonyesha.

Na huko kusema kwao "Hakuna hata mahala pamoja katika maandiko yote ya Kiarabu panapoweza kuonyeshwa palipo na tamko hili limetumiwa kwa maana nyingine".

Tazama kutokuwa na haya kwa Makadiyani. Wanamwona hapo *Az Zamakhshary* kwenye *Mutawaffyka* anavyotaja tafsiri zote za tamko hilo linapotumika hivyo. Na wanamwona huyo Al Alusy alivyozibainisha tafsiri zake zote hizi; linapotumika hivyo. Na wamemwona mwenye *Al Mufradat* alivyozitaja tafsiri zake zote; bali akasema pia kuwa kulifasiri kwa kufa sio maana yake ya asili. Na wamemwona mwenye *Al Qamus* pia alivyotaja tafsiri zake zote. Na mwenye *Al Munjid* kadhalika. Wanajua Makadiyani yanayosemwa na watu na wanayoyasema wao; lakini wanadanganya tu MAKUSUDI.

Na amesema mwenye *Al Mufradat* katika kulifasiri hilo tamko la *Mutawaffyka* kuwa: Ibnu Abbas amelifasiri hivi: "Kuwa alimfisha kisha akamfufua." Si huyu mwenye Mufradat ambaye wanajidai wanafuata yaliyomo katika kitabu chake hicho? Wanamwona anasema kuwa Ibn Abbas kafasiri kuwa atamfisha kisha atamfufua, tena ampandishe mbinguni.

Na huko kushadidia kwao kuwa Ibn Abbas kafasiri katika *Al Bukhary* (*Mutawaffyka* = Nitakufisha hakuwasaidii kitu kwa wanaojua. Watawadanganya kwa kuwapoteza wasiojua. Wanaojua wanajua kuwa Hadithi za *Al Bukhary* haziambiwi SAHIHI ila zile anazozitajia Isnadi yaani anazosema "Nimemsikia Fulani, na Fulani kamsikia Fulani", mpaka mwisho. Na hiyo tafsiri ya Ibn Abbas hakuitajia isnadi, kama wanavyoona. Kasema hivi tu "Kasema Ibn Abbas maana yake nitakufisha". Ama hao wengine aliowataja ni uwongo tu.

Na wakamtaja Sheikh Shaltuti wakampa sifa zake zote, na moja katika hizo ni kuwa yeye ni mwanachama wa Halmashauri ya kutoa Fatwa katika Chuo Kikuu cha Al Azhar. Kweli si uwongo. Uwongo waliouficha ni kule kuficha kwao kuwa Fatwa yake hiyo haikubaliwi kabisa na hao Halmashauri wenziwe; na ndio maana wakaizuilia kabisa Fatwa hiyo kutoka katika gazeti la Al Azhar la kutaja Fatwa za dini na mambo mengine ya Dini linaloitwa Majallatul Azhar; wala haikukubaliwa pia kutoka katika magazeti mengine ya dini ya huko Misr, kama Nurul Islam, Liwaul Islam, Hadyun Nabawiy na mengineyo. Ikatoka katika gazeti la mambo yasiyokuwa ya dini — gazeti linaloitwa *Ar Risalatu War Riwayah*. Gazeti hili lilokhusika na hadithi za upuuzi na za uwongo. Na wao Makadiyani ndio waliomshika Shaltut aandike hayo. Na wenyewe wanajua, na kila mtu anajua.

Na wakajidai Makadiyani kutaja kitabu kinachoitwa Fat-hul Bayani na wakataja yaliyomo humo. Wanajidai kudhanisha watu kuwa kitabu hicho ni cha mwanachuoni wa Kislamu mkubwa; kumbe chuo chao wenyewe Makadiyani. Bidhaa yao wenyewe mbovu.

Na Hadithi za kuwa Nabii Isa atateremka kutoka mbinguni kuja tena ulimwenguni zimetajwa katika vitabu vyote SAHIHI vya Hadithi hata hiyo *Al Bukhary* kama ilivyo papo hapo kwenye hiyo habari ya *Mutawaffyka*. Lakini ni watu wabaya kweli kweli hawa — kitu huwako papo hapo wakakirusha na wakajikurupusha nacho

56. Ama wale waliokufuru, nitawaadhibu adhabu kali katika dunia na Akhera, wala hawatapata wasaidizi (wa kuwasaidia).

فأما الذين كفروا فأعذبهم عذابا شديدا
في الدنيا والآخرة وما لهم من نصرين ﴿٥٦﴾

57. Na ama wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, basi (Mwenyezi Mungu) atawalipa ujira wao (kamili). Na Mwenyezi Mungu hawapendi madhalimu.

وأما الذين آمنوا وعملوا الصلحت فيوفيهم
أجورهم والله لا يحب الظلمين ﴿٥٧﴾

58. Haya tunayokusomea ni katika Aya na mauidha yenye hikima (kubwa).

ذلك نتلوه عليك من الآيت والذكر الحكيم ﴿٥٨﴾

59. Bila shaka hali ya Isa kwa Mwenyezi Mungu ni kama hali ya Adam; alimwumba kwa udongo kisha akamwambia: "Kuwa"; basi akawa.

إن مثل عيسى عند الله كمثل آدم خلقه من
تراب ثم قال له كن فيكون ﴿٥٩﴾

60. (Hii) ni haki inayotoka kwa Mola wako. Basi usiwe miongoni mwa wanaofanya shaka.

الحق من ربك فلا تكن من الممترين ﴿٦٠﴾

61. Watakaokuhoji (sasa) katika haya baada ya kukufikilia ilimu (hii na kuwafikilia wao), waambie: "Njooni tuwaite watoto wetu na watoto wenu; na wanawake wa kwetu na wanawake wa kwenu, na sisi na nyinyi; kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo."

فمن حاجك فيه من بعد ما جاءك من
العلم فقل تعالوا ندع أبناءنا وأبناءكم
ونساءنا ونساءكم وأنفسنا وأنفسكم
ثم نبتهل فنجعل لعنت الله على الكذبين ﴿٦١﴾

62. Kwa yakini haya ndiyo maelezo ya kweli. Na hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu; na kwa hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye nguvu na Mwenye hikima.

إن هذا لهو القصص الحق وما من إله إلا
الله وإن الله لهو العزيز الحكيم ﴿٦٢﴾

63. Na kama wakikengeuka, (Mwenyezi Mungu atawatia adabu), kwani Mwenyezi Mungu anawajua waharibifu.

فإن تولوا فإن الله عليم بالمفسدين ﴿٦٣﴾ ع

64. Sema: "Enyi watu mliopewa Kitabu (cha Mwenyezi Mungu. Mayahudi na Manasara)! Njooni katika neno lililo sawa baina yetu na baina yenu: ya kwamba tusimwabudu yo yote ila Mwenyezi Mungu,

قل يأهل الكتب تعالوا إلى كلمة سواء

---

kusudi, ili wazidi kupoteza Waislamu. Ama hawa maadui sana kwa Waislamu.

Katika uwongo wao wameandika: "Quran imevunja kabisa itikadi hii ya kupanda Isa hai mbinguni katika Aya zisizopunguwa 30." Eee, Uwongo wa Makadiyani! Kwa nini wasitutajie walau moja katika hizo! Hawajali hata chembe watu hawa kusema uwongo hata ulio dhahiri usiokuwa na mafundo hata chembe! Kani yao kubwa kabisa ni katika kutaka kuwapotoa Waislamu na itikadi zao. Na tumeongeza kutaja habari hii katika Aya ya 117 ya *Suratul Maaida*, Juzuu ya Sabaa.

59. Kupotoka kwa Manasara katika Nabii Isa hata wakamwitakidi kuwa ni mtoto wa Mwenyezi Mungu na kumwabudu — ati kwa ajili kazaliwa na mama tu pasina baba. Basi kwa nini hawamuitakidi Nabii Adam kuwa mtoto wa Mwenyezi Mungu vile vile kwani na yeye ni vile vile kama Nabii Isa — kaumbika bila ya baba; bali na bila ya mama pia?

61. Sasa ilivyokuwa hoja zote zimebainishwa dhahir shahir — na hao Manasara (na Mayahudi) hawataki tu kuamini — basi wanaambiwa wakusanyike pamoja na Mtume, na waapize kuwa aliye mwongo limfike hili na hili na . . . Basi Mtume aliwatajia shauri hili. Lakini waliogopa wakalikataa; ikadhihiri kwa watu wote kuwa ni waongo kweli..

بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا اللَّهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهِ
شَيْئًا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِنْ
دُونِ اللَّهِ ۚ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَقُولُوا اشْهَدُوا بِأَنَّا
مُسْلِمُونَ ﴿٦٤﴾

wala tusimshirikishe (Mwenyezi Mungu) na cho chote; wala baadhi yetu tusiwafanye wengine kuwa waungu badala ya Mwenyezi Mungu (au pamoja na Mwenyezi Mungu). Wakikengeuka, semeni: "Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu, (tumenyenyekea amri za Mwenyezi Mungu)."

يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لِمَ تُحَاجُّونَ فِي إِبْرَاهِيمَ وَمَا
أُنْزِلَتِ التَّوْرَاةُ وَالْإِنْجِيلُ إِلَّا مِنْ بَعْدِهِ ۚ
أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٦٥﴾

65. Enyi watu mliopewa Kitabu! Mbona mnabishana juu ya Ibrahimu, na hali Taurati na Injili havikuteremshwa ila baada yake? Basi je, hamfahamu?

هَا أَنْتُمْ هَٰؤُلَاءِ حَاجَجْتُمْ فِيمَا لَكُمْ بِهِ عِلْمٌ فَلِمَ
تُحَاجُّونَ فِيمَا لَيْسَ لَكُمْ بِهِ عِلْمٌ ۚ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَ
أَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٦٦﴾

66. Angalieni. Nyinyi mlibishana katika yale mliyoyajua. Mbona (sasa) mnabishana katika yale msiyoyajua? Na Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye, nyinyi hamjui (kitu).

مَا كَانَ إِبْرَاهِيمُ يَهُودِيًّا وَلَا نَصْرَانِيًّا وَلَٰكِنْ
كَانَ حَنِيفًا مُسْلِمًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٦٧﴾

67. Ibrahimu hakuwa Myahudi wala Mkristo, lakini alikuwa mwongofu, mtii; wala hakuwa katika washirikina.

إِنَّ أَوْلَى النَّاسِ بِإِبْرَاهِيمَ لَلَّذِينَ اتَّبَعُوهُ وَهَٰذَا
النَّبِيُّ وَالَّذِينَ آمَنُوا ۗ وَاللَّهُ وَلِيُّ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٨﴾

68. Watu wanaomkurubia zaidi Ibrahimu ni wale waliomfuata yeye (katika zama zake) na Mtume huyu (Muhammad) na waliomwamini (Mtume huyu). Na Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi wa wenye kuamini.

وَدَّتْ طَائِفَةٌ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَوْ
يُضِلُّونَكُمْ وَمَا يُضِلُّونَ إِلَّا أَنْفُسَهُمْ وَمَا
يَشْعُرُونَ ﴿٦٩﴾

69. Baadhi ya waliopewa Kitabu wanapenda wakupotezeni; lakini hawapotezi ila nafsi zao, na (hali wenyewe) hawatambui.

يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لِمَ تَكْفُرُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ
وَأَنْتُمْ تَشْهَدُونَ ﴿٧٠﴾

70. Enyi mliopewa Kitabu! Mbona mnazikataa Aya za Mwenyezi Mungu, hali mnajua (kuwa ndiyo ndizo)?

يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لِمَ تَلْبِسُونَ الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ وَتَكْتُمُونَ
الْحَقَّ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٧١﴾ ع

71. Enyi mliopewa Kitabu! Mbona mnachanganya haki na batili, na mnaficha haki, hali mnajua?

وَقَالَتْ طَائِفَةٌ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ آمِنُوا
بِالَّذِي أُنْزِلَ عَلَى الَّذِينَ آمَنُوا وَجْهَ النَّهَارِ

72. Na baadhi ya wale waliopewa Kitabu walisema (kuwaambia wenzao): "Yaaminini yale waliyoteremshiwa Waislamu. (Yaaminini) mwanzo

---

65. Mayahudi na Manasara, kila mmoja katika hawa anajinasibishia Nabii Ibrahimu kuwa ni Mtume wake, na hali ya kuwa Mayahudi kitabu chao ni Taurati (Na Taurati si ya Nabii Ibrahimu bali ya Nabii Musa). Na Manasara kitabu chao ni Injili (Na Injili si ya Nabii ibrahimu bali ni ya Nabii Isa.) Basi haya yanafahamisha kuwa hao (a) Hawafahamu kitu, wanajisemea tu au (b) Wanajitia pambani makusudi.

68. Kwani dini aliyokuja nayo Nabii Ibrahimu inawafikiana kabisa na aliyokuja nayo Nabii Muhammad. Na hiyo ya Nabii Musa na ya Nabii Isa ilikuwa vivi hivi kabla ya kuharibiwa na Mayahudi na Manasara.

72. Miongoni mwa vitimbi walivyokuwa wakivifanya Mayahudi na Manasara ili kuwabaidisha watu na dini ya haki — ya Uislamu — ni kuwaamrisha baadhi yao kwenda kusilimu kisha kurtadi (kurejea katika dini yao) ili

وَاكْفُرُوٓا ءَاخِرَهُۥ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٧٢﴾

wa mchana na yakataeni mwisho wake (mwisho wa mchana); huenda watarejea."

وَلَا تُؤْمِنُوٓا إِلَّا لِمَن تَبِعَ دِينَكُمْ قُلْ إِنَّ الْهُدَىٰ
هُدَى اللَّهِ أَن يُؤْتَىٰٓ أَحَدٌ مِّثْلَ مَآ أُوتِيتُمْ أَوْ
يُحَآجُّوكُمْ عِندَ رَبِّكُمْ قُلْ إِنَّ الْفَضْلَ بِيَدِ اللَّهِ
يُؤْتِيهِ مَن يَشَآءُ وَاللَّهُ وَٰسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٧٣﴾

73. "Wala msimwamini ila yule anayefuata dini yenu." (Mwenyezi Mungu akasema kumwambia Mtume) Sema: "Bila shaka uwongozi khasa ni uwongozi wa Mwenyezi Mungu." (Walisema hao waliopewa Kitabu kuwaambia wenzao: "Wala msiamini) kuwa atapewa mmojawapo mfano wa yale mliyopewa nyinyi (Mayahudi na Manasara); au watakuhojini mbele ya Mola wenu." (Mwenyezi Mungu akasema kumwambia Mtume) Sema: "Hakika fadhila zi katika mkono wa Mwenyezi Mungu, humpa amtakaye; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa (na) ajuaye "

يَخْتَصُّ بِرَحْمَتِهِۦ مَن يَشَآءُ وَاللَّهُ
ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿٧٤﴾

74. Humchagua kwa (kumpa) rehema Zake amtakaye; na. Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye fadhila kubwa."

وَمِنْ أَهْلِ الْكِتَٰبِ مَنْ إِن تَأْمَنْهُ بِقِنطَارٍ يُؤَدِّهِۦٓ إِلَيْكَ
وَمِنْهُم مَّنْ إِن تَأْمَنْهُ بِدِينَارٍ لَّا يُؤَدِّهِۦٓ إِلَيْكَ إِلَّا
مَا دُمْتَ عَلَيْهِ قَآئِمًا ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا لَيْسَ
عَلَيْنَا فِى الْأُمِّيِّۦنَ سَبِيلٌ وَيَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ
الْكَذِبَ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿٧٥﴾

75. Na katika waliopewa Kitabu kuna ambao ukiwapa amana ya mrundi wa mali watakurudishia. Na katika wao kuna ambao ukiweka kwao amana ya dinari moja (tu hivi) hawakurudishii, isipokuwa uendelee kuwasimamia (kuwadai). Haya ni kwa sababu walisema: "Hapana njia juu yetu (ya kulaumiwa) kwa (ajili) ya hawa wajinga (watu wasiokuwa dini moja na sisi)." Na wanasema uwongo juu ya Mwenyezi Mungu, hali wanajua (kuwa sivyo hivyo).

بَلَىٰ مَنْ أَوْفَىٰ بِعَهْدِهِۦ وَاتَّقَىٰ فَإِنَّ اللَّهَ
يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ ﴿٧٦﴾

76. Sivyo hivyo (wanavyosema. Lakini) anayetekeleza ahadi yake na akajilinda (na dhambi, atakuwa kipenzi cha Mwenyezi Mungu), na Mwenyezi Mungu huwapenda wajilindao (na madhambi).

إِنَّ الَّذِينَ يَشْتَرُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَأَيْمَٰنِهِمْ ثَمَنًا
قَلِيلًا أُولَٰٓئِكَ لَا خَلَٰقَ لَهُمْ فِى الْءَاخِرَةِ وَلَا
يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ وَلَا يَنظُرُ إِلَيْهِمْ يَوْمَ الْقِيَٰمَةِ

77. Hakika wale wanaouza ahadi ya Mwenyezi Mungu na viapo vyao kwa ajili ya thamani ndogo ya kilimwengu hao ndio hawatakuwa na sehemu ya kheri katika Akhera, wala Mwenyezi Mungu hatasema nao (maneno mazuri) wala hatawatazama (jicho la rehema) siku hiyo ya Kiyama, wala

---

wawatie wasiwasi na wahka wale Waislamu wa kweli, waone 'Labda si dini ya haki hii. Mbona wameingia mahodari wale, kisha wakatoka?' Lakini bure; khadaa zao hazikufaa kitu.

75. Hapa Mwenyezi Mungu anafedhehi uwongo wa Mayahudi na wa Manasara. Wao walikuwa wakisema kuwa Mwenyezi Mungu kawapa ruhusa wale mali ya watu wasiokuwa dini moja na wao. Ni uwongo kabisa. Mwenyezi Mungu hakubalishi dhulma — ya kudhulumiwa yo yote yule awaye. Mungu hakutoa ruhusa hiyo.

Na wako Waislamu wajinga wanaoamini haya — ya kuwa Mwislamu inamjuzia kula haki ya asiyekuwa Mwislamu. Uwongo. Asiamini mtu hivi.

77-78. Hapa panatajwa hilaki itakayowakuta hawa wanaodanganya watu kwa jina la dini, wakawasomea watu maneno ya uwongo, na huku wanasingizia kuwa ni ya Mwenyezi Mungu — ili wapate mali kwao na Jaha; kama hao wanaowasomea watu maneno ya uwongo ya Manazili ya kuolea na mengineyo, na ya faida za Matanga, na

وَلَا يُزَكِّيهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٧٧﴾

hatawatakasa (na madhambi yao); nao watapata adhabu iumizayo.

وَإِنَّ مِنْهُمْ لَفَرِيقًا يَلْوُونَ أَلْسِنَتَهُمْ بِالْكِتَابِ
لِتَحْسَبُوهُ مِنَ الْكِتَابِ وَمَا هُوَ مِنَ الْكِتَابِ
وَيَقُولُونَ هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ وَمَا هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ
وَيَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿٧٨﴾

78. Na miongoni mwao kuna baadhi yao wanaopinda ndimi zao kwa (kusoma) kitabu ili mpate kuyafikiri (maneno) yao hayo kuwa ni ya Kitabu (cha Mwenyezi Mungu); wala si ya Kitabu (cha Mwenyezi Mungu), na wanasema: "Haya yametoka kwa Mwenyezi Mungu", na hali hayakutoka kwa Mwenyezi Mungu; na wanamsingizia Mwenyezi Mungu uwongo na hali wanajua (kuwa huo ni uwongo).

مَا كَانَ لِبَشَرٍ أَنْ يُؤْتِيَهُ اللَّهُ الْكِتَابَ وَالْحُكْمَ
وَالنُّبُوَّةَ ثُمَّ يَقُولَ لِلنَّاسِ كُونُوا عِبَادًا لِي مِنْ
دُونِ اللَّهِ وَلَٰكِنْ كُونُوا رَبَّانِيِّينَ بِمَا كُنْتُمْ تُعَلِّمُونَ
الْكِتَابَ وَبِمَا كُنْتُمْ تَدْرُسُونَ ﴿٧٩﴾

79. Haiwi kwa mtu ambaye Mwenyezi Mungu amempa Kitabu na hukumu na Unabii aseme kuwaambia watu: "Kuweni wa kuniabudu mimi badala ya Mwenyezi Mungu (peke yake)". Bali (yeye atawaambia). "Kuweni wenye kuabudu Mwenyezi Mungu. Kwa sababu mnafundisha Kitabu na kwa sababu mnakisoma"

وَلَا يَأْمُرَكُمْ أَنْ تَتَّخِذُوا الْمَلَائِكَةَ وَالنَّبِيِّينَ أَرْبَابًا
أَيَأْمُرُكُمْ بِالْكُفْرِ بَعْدَ إِذْ أَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿٨٠﴾ ع

80. Wala hatakuamrisheni kuwafanya Malaika na Manabii kuwa waungu. Je, atakuamrisheni ukafiri baada ya kuwa nyinyi Waislamu?

وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ النَّبِيِّينَ لَمَا آتَيْتُكُمْ مِنْ
كِتَابٍ وَحِكْمَةٍ ثُمَّ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مُصَدِّقٌ لِمَا
مَعَكُمْ لَتُؤْمِنُنَّ بِهِ وَلَتَنْصُرُنَّهُ قَالَ أَأَقْرَرْتُمْ وَ
أَخَذْتُمْ عَلَىٰ ذَٰلِكُمْ إِصْرِي قَالُوا أَقْرَرْنَا قَالَ
فَاشْهَدُوا وَأَنَا مَعَكُمْ مِنَ الشَّاهِدِينَ ﴿٨١﴾

81. Na (kumbukeni) alipochukua Mwenyezi Mungu ahadi kwa Manabii (akawaambia): "Nikisha kupeni Kitabu na hikima, kisha akakujieni Mtume msadikishaji wa yale yaliyo pamoja nanyi, ni juu yenu kumwamini na kumsaidia." Akasema: (Mwenyezi Mungu) "Je, mmekiri na mmekubali kushika agizo langu juu ya hayo?" Wakasema: "Tumekubali." Akasema: "Basi shuhudieni, na Mimi ni pamoja nanyi katika mashahidi."

فَمَنْ تَوَلَّىٰ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٨٢﴾

82. Basi watakaokengeuka baada ya haya, (Mwenyezi Mungu atawaadhibu kwani) hao ndio wavunjao amri.

---

kuwa Mtume kataja fadhila za kusoma Maulidi, na pia Masahaba wake wametaja, na yaliyo kama haya. Wanajua kuwa ni uwongo, lakini hawataki pato hilo liwakose. Wanakhitari thamani ndogo ya kiduniani na kupata adhabu ya Akhera.

79. Hapa wanavunjwa Mayahudi wanaojidai kuwa Sayyidna Uzayr kawaamrisha wamwabudu. Na wanavunjwa Manasara wanaosema kuwa Sayyidna Isa kawaamrisha wamwabudu.

81. Hapo zamani — kabla ya kuja Nabii Muhammad — wakiwako Mitume wawili watatu wakati mmoja nchi moja au nchi mbali mbali, kama Nabii Ibrahimu na Nabii Luti, Nabii Ismaili na Nabii Is-haqa, Nabii Musa na Nabii Haruni. Nabii Yahya na Nabii Isa, na kama hao. Basi walipewa ahadi watiane nguvu, wasipingane wakahusudiana.

Basi na namna hivi ndivyo wanavyoambiwa wanavyuoni — kuwa wasiwapinge wenziwao maadam wamo katika haki. Lakini wapi! Wengi katika hao husuda haiwaachii. Hao Mitume ndio walioifuata amri. Na sisi tumeambiwa kuwa Mitume wawe ndio ruwaza zetu za kuigia. Basi natuige mambo yetu kwa ruwaza hizo, au tutapotea. Tuwache kusema uwongo katika dini kwa ajili ya kuchukiana.

83. Je! Wanataka dini isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu, na hali kila kilichomo mbinguni na ardhini kinamtii Yeye, kikipenda kisipende? Na Kwake watarejeshwa wote.

أفغير دين الله يبغون وله أسلم من في السموت والأرض طوعا وكرها وإليه يرجعون ﴿٨٣﴾

84. Sema: "Tumemwamini Mwenyezi Mungu, na yale tuliyoteremshiwa na aliyoteremshiwa Ibrahimu na Ismaili na Ishaka na Yakubu na watoto (wake), na yale aliyopewa Musa na Isa na Manabii (wengine) kutoka kwa Mola wao. Hatubagui baina yao hata mmoja, na sisi tunanyenyekea Kwake.

قل آمنا بالله وما أنزل علينا وما أنزل على إبرهيم وإسمعيل وإسحق ويعقوب والأسباط وما أوتي موسى وعيسى والنبيون من ربهم لا نفرق بين أحد منهم ونحن له مسلمون ﴿٨٤﴾

85. Na anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye khasara (kubwa kabisa).

ومن يبتغ غير الإسلام دينا فلن يقبل منه وهو في الآخرة من الخسرين ﴿٨٥﴾

86. Mwenyezi Mungu atawaongozaje (kwendea haki) watu waliokufuru baada ya kuamini kwao, na wakashuhudia ya kwamba Mtume (huyu) ni wa haki, na zikawafikia hoja zilizo wazi? Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu.

كيف يهدي الله قوما كفروا بعد إيمانهم وشهدوا أن الرسول حق وجاءهم البينت والله لا يهدي القوم الظلمين ﴿٨٦﴾

87. Hao malipo yao ni kuwa iko juu yao laana ya Mwenyezi Mungu, na ya Malaika na ya watu wote

أولئك جزاؤهم أن عليهم لعنة الله والملئكة والناس أجمعين ﴿٨٧﴾

88. Humo watakaa milele. Hawatapunguziwa adhabu wala hawatapewa nafasi (ya kupumzika)

خلدين فيها لا يخفف عنهم العذاب ولا هم ينظرون ﴿٨٨﴾

89. Isipokuwa wale waliotubu baada ya hayo na wakatengeneza (amali zao). (Hao Mungu atawasamehe) kwani Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

إلا الذين تابوا من بعد ذلك وأصلحوا فإن الله غفور رحيم ﴿٨٩﴾

90. Hakika wale waliokufuru baada ya kuamini kwao, kisha wakazidi kukufuru; toba yao haitakubaliwa (kamwe), na hao ndio waliopotea (kweli kweli).

إن الذين كفروا بعد إيمانهم ثم ازدادوا كفرا لن تقبل توبتهم وأولئك هم الضالون ﴿٩٠﴾

91. Hakika wale waliokufuru, na wakafa hali ni makafiri, basi haitakubaliwa kwa mmoja wao ijapokuwa katoa fidia ya dhahabu kwa kuijaza ardhi yote. Hao ndio watakaopata adhabu iumizayo, wala hawatakuwa na wasaidizi.

إن الذين كفروا وماتوا وهم كفار فلن يقبل من أحدهم ملء الأرض ذهبا ولو افتدى به أولئك لهم عذاب أليم وما لهم من نصرين ﴿٩١﴾

92. Hamtaweza kuufikia wema (khasa) mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda; na cho chote mnachokitoa, basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua.

لن تنالوا البر حتى تنفقوا مما تحبون وما تنفقوا من شيء فإن الله به عليم ﴿٩٢﴾

---

84. Hii ndiyo itikadi ya Uislamu kama tulivyobainisha katika maelezo ya Aya ya mwisho ya *Suratil Baqarah.*

92. Cho chote cha kheri anachokitoa mtu katika njia za kheri anapata thawabu. Lakini kila anapotoa anachokipenda zaidi ndio bora. Ukimpa masikini nguo usiyoitaka utapata thawabu. Lakini ukimpa unayoitaka utapata thawabu zaidi.

93. Kila chakula kilikuwa halali kwa kizazi cha Israili (Mayahudi) isipokuwa kile alichojiharimishia Israili mwenyewe — kabla haijateremshwa Taurati. Sema: "Leteni hiyo Taurati muisome ikiwa mnasema kweli."

كُلُّ الطَّعَامِ كَانَ حِلًّا لِّبَنِيٓ إِسْرَٰٓءِيلَ إِلَّا مَا
حَرَّمَ إِسْرَٰٓءِيلُ عَلَىٰ نَفْسِهِۦ مِن قَبْلِ أَن تُنَزَّلَ
التَّوْرَىٰةُ ۗ قُلْ فَأْتُوا بِالتَّوْرَىٰةِ فَاتْلُوهَآ إِن كُنتُمْ
صَٰدِقِينَ ﴿٩٣﴾

94. Na wo wote watakaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu baada ya haya, basi hao ndio madhalimu (wa nafsi zao).

فَمَنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ مِنۢ بَعْدِ ذَٰلِكَ
فَأُولَٰٓئِكَ هُمُ الظَّٰلِمُونَ ﴿٩٤﴾

95. Sema: "Mwenyezi Mungu amesema kweli." Basi fuateni mila ya Ibrahimu aliyekhalisika (na nyendo za upotofu), wala hakuwa miongoni mwa washirikina.

قُلْ صَدَقَ اللَّهُ ۗ فَاتَّبِعُوا مِلَّةَ إِبْرَٰهِيمَ
حَنِيفًا ۖ وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٩٥﴾

96. Kwa yakini Nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu (kufanya ibada) ni ile iliyoko Makka, yenye baraka na uwongozi kwa ajili ya walimwengu wote.

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبَارَكًا
وَهُدًى لِّلْعَٰلَمِينَ ﴿٩٦﴾

97. Humo mna Ishara zilizo wazi (za kuonyesha utukufu wake na ukongwe wake. Miongoni mwa hizo ni) mahali alipokuwa akisimama Ibrahimu, na anayeingia (nchi hiyo) anakuwa katika salama. Na Mwenyezi Mungu amewawajibishia watu wafanye Hija katika Nyumba hiyo; yule awezaye kufunga safari kwenda huko. Na atakayekanusha (asende, na hali ya kuwa anaweza) basi Mwenyezi Mungu si mhitaji kuwahitajia walimwengu.

فِيهِ ءَايَٰتٌۢ بَيِّنَٰتٌ مَّقَامُ إِبْرَٰهِيمَ ۖ وَمَن دَخَلَهُۥ
كَانَ ءَامِنًا ۗ وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ
اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا ۚ وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ
عَنِ الْعَٰلَمِينَ ﴿٩٧﴾

98. Sema: "Enyi watu mliopewa Kitabu! Kwa nini mnazikataa hoja za Mwenyezi Mungu, hali Mwenyezi Mungu ni shahidi juu ya yote mnayoyatenda?

قُلْ يَٰٓأَهْلَ الْكِتَٰبِ لِمَ تَكْفُرُونَ بِـَٔايَٰتِ اللَّهِ
وَاللَّهُ شَهِيدٌ عَلَىٰ مَا تَعْمَلُونَ ﴿٩٨﴾

99. Sema: "Enyi mliopewa Kitabu! Kwa nini mnawazuilia (watu) na njia (dini) ya Mwenyezi Mungu; wale walioamini? Mkaitafutia kosa, na hali mnashuhudia (kuwa ni njia ya Mwenyezi Mungu isiyokuwa na kosa). Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na mnayoyatenda."

قُلْ يَٰٓأَهْلَ الْكِتَٰبِ لِمَ تَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ
اللَّهِ مَنْ ءَامَنَ تَبْغُونَهَا عِوَجًا وَأَنتُمْ
شُهَدَآءُ ۗ وَمَا اللَّهُ بِغَٰفِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٩٩﴾

100. Enyi mlioamini! Mkiwatii baadhi ya wale waliopewa Kitabu, watakurudisheni kuwa makafiri baada ya Uislamu wenu.

يَٰٓأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوٓا إِن تُطِيعُوا فَرِيقًا مِّنَ
الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَٰبَ يَرُدُّوكُم بَعْدَ إِيمَٰنِكُمْ
كَٰفِرِينَ ﴿١٠٠﴾

101. Na mnakanushaje, hali nyinyi mnasomewa Aya za Mwenyezi Mungu, na Mtume wake yuko

وَكَيْفَ تَكْفُرُونَ وَأَنتُمْ تُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ ءَايَٰتُ

---

93. Mayahudi walimwambia Mtume "Wewe hufuati mwendo wa Nabii Ibrahimu ingawa unajidai unafuata. Mbona unakula nyama ya ngamia; na Nabii Ibrahimu hakuwa akila nyama ya ngamia?" Ndiyo wanasutwa hapa kuwa: Ni uwongo huo; na dalili ni hiyo Taurati. Nawaifungue hiyo Taurati wataona kuwa Nabii Yaaqubu (Israili) — si Nabii Ibrahimu — ndiye aliyejiharimishia kula nyama ya ngamia mwenyewe kwa nafsi yake bila ya kulazimishwa na Mwenyezi Mungu.

96. Hapa inabainishwa kuwa nyumba ya mwanzo iliyowekewa watu kufanya Ibada ni Al Kaaba, si Baytil Muqaddas, kama walivyokuwa wakidai Mayahudi. Na alama ya haya ni hizo dalili zilizotajwa.